# BUNGE LA TANZANIA

# MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KWANZA

## Kikao cha Nne – Terehe 20 Novemba, 2015

*(Kikao Kilianza Saa 9.00 Alasiri)*

## D U A

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia A. Mwansasu) Alisoma Dua*

## KIAPO CHA UAMINIFU

Mheshimiwa Mbunge afuataye aliapa Kiapo cha Uaminifu:-

Mhe. Suleiman Masoud Nchambi

## TAARIFA YA SPIKA

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba kutoa taarifa kwamba Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa John Pombe Joseph Magufuli, ameamua kulihutubia Bunge hili leo tarehe 20 Novemba, 2015 kwa mujibu wa Ibara ya 91(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ambayo inampa mamlaka ya kulihutubia Bunge jipya katika Mkutano wake wa Kwanza na kulifungua rasmi. Shughuli hiyo ya Mheshimiwa Rais kulihutubia Bunge na kufanya ufunguzi rasmi itafanyika saa kumi jioni hii.

Waheshimiwa Wabunge, wakati tukisubiri muda huo ufike, nina matangazo machache. Tangazo la kwanza linahusu Tamko la Viongozi wa Umma kuhusu rasilimali na madeni, fomu ziko ofisi ya Mheshimiwa Spika. Tafadhali mzichukue na mzijaze kwa wakati kwa sababu sheria inatutaka kufanya hivyo. Hilo ni tangazo letu la kwanza na hiyo ni kwa mujibu wa Ibara ya 70 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na pia vifungu vya (9) na (11) vya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma ya mwaka 1995.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo la pili, kuna ambao hawajarudisha Fomu za Maelezo Binafsi. Tunawaomba warudishe fomu hizo kabla hawajaondoka Dodoma ili kuweza kutusaidia katika kufanya mipango mingine.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo la tatu linawahusu wale ambao hawajarudisha Fomu za Maombi ya Kamati. Kuwa mjumbe wa Kamati lazima ulete maombi na fomu hizo Waheshimiwa Wabunge mlipewa, tunaomba mzirejeshe ili muweze kuturahisishia kazi ya kuwapangia Kamati.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo, sasa namuita Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya shughuli inayofuata. Mwanasheria Mkuu wa Serikali, karibu. *(Makofi)*

## HOJA YA KUTENGUA KANUNI ZA BUNGE

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika:-

KWA KUWA, moja ya shughuli zilizopangwa katika Orodha ya Shughuli za leo, ni Ufunguzi Rasmi wa Bunge Jipya la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania utakaofanywa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye atalihutubia na kulifungua Rasmi Bunge Jipya kwa mujibu wa Ibara ya 91(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na Kanuni 26(2) na 23(1)(h) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013;

NA KWA KUWA, Mheshimiwa Spika amewaalika viongozi mbalimbali kuja kusikiliza hotuba ya Mheshimiwa Rais wakati akihutubia na kulifungua Rasmi Bunge Jipya la Kumi na Moja la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

NA KWA KUWA, kwa kutambua kwamba Kanuni ya 139(1) na 143(f) zinaelekeza kwamba wageni wanaoruhusiwa kuingia Bungeni watakaa maeneo maalum yaliyotengwa kwa ajili yao, inabidi Bunge litengue Kanuni hizi ili kuruhusu viongozi walioalikwa na Mheshimiwa Spika kuingia na kukaa ndani ya ukumbi wa Bunge;

HIVYO BASI, Bunge linaazimia kwamba kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa shughuli za Bunge katika Mkutano huu wa Kwanza wa Bunge la Kumi na Moja, Kanuni ya 139(1) na 143(f) zitenguliwe kama ifuatavyo:-

Kanuni ya 139(1) na 143(f) ambazo kwa ujumla wake zinaelekeza kwamba wageni walioruhusiwa kuingia Bungeni watakaa maeneo maalum yaliyotengwa kwa ajili yao zitenguliwe na badala yake Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mheshimiwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mheshimiwa Jaji Mkuu wa Tanzania, Mheshimiwa Jaji Mkuu wa Zanzibar na Mheshimiwa Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar waruhusiwe kuingia na kukaa sehemu watakazopangiwa ndani ya ukumbi wa

Bunge kwa ajili ya kusikiliza hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati akihutubia na kulifungua Rasmi Bunge Jipya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono, sasa nitawahoji.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika…

**NAIBU SPIKA:** Wanaokubali…

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tundu Lissu naomba ukae.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tundu Lissu nimesimama naomba ukae. *(Makofi)*

Sasa nitawahoji wanaokubali hoja ya Mwanasheria Mkuu waseme ndiyo.

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo!

**WABUNGE FULANI:** Mwongozo.

**WABUNGE FULANI:** Kuhusu utaratibu.

**WABUNGE FULANI:** Hakuna, hakuna.

**NAIBU SPIKA:** Wasiokubali waseme siyo.

**WABUNGE FULANI:** Siyo!

**NAIBU SPIKA:** Nadhani waliosema ndiyo wameshinda. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Aaaaaah!

**NAIBU SPIKA:** Kwa hiyo, Bunge limeafiki viongozi wa Kitaifa waliotajwa katika hoja ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali…

**MBUNGE FULANI:** Utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Waingie ndani ya ukumbi wa Bunge wakati wa ufunguzi Rasmi wa Bunge utakaofanywa na Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Hoja ya Viongozi wa Kitaifa waliotajwa kuruhusiwa kuingia ndani ya ukumbi wa Bunge wakati wa ufunguzi Rasmi wa Bunge Jipya ilipitishwa na Bunge)*

**MBUNGE FULANI:** Tutoke nje.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, utaratibu utakaofuata ni kwamba Mheshimiwa Rais atakapofika ama atakapokaribia kufika tutataarifiwa halafu mimi nitatoka ili niende kumpokea. Kwa hiyo, tutaahirisha Bunge kwa muda mfupi ili tuweze kumpokea Mheshimiwa Rais na kumuingiza ndani ya ukumbi wa Bunge. Naomba tuvute …

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mwongozo wa Spika tafadhali.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tundu Lissu. *(Makofi)*

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) inayoruhusu Mbunge kuomba Mwongozo endapo kuna jambo limetokea Bungeni mapema ili Spika alitolee ufafanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa kanuni na taratibu za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda tupate Mwongozo wa Kiti chako kuhusu baadhi ya wageni ambao uamuzi umetolewa hapa wa kuwakaribisha ndani ya ukumbi wa Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hali ilivyo leo hatuna Rais halali wa Zanzibar. Kwa hali ilivyo leo hatuna Makamu wa Kwanza au wa Pili halali wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Kwa hali ilivyo leo hatuna Spika wa Baraza la Wawakilishi wala Baraza la Wawakilishi lenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuna viongozi hawa ambao nimewataja kwa sababu kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar, Ibara ya 28(2) muda wa madaraka ya Rais wa Zanzibar na Serikali yake uliisha tangu tarehe 2 Novemba, 2015. Ibara hiyo ya Katiba ya Zanzibar kinaeleza wazi kwamba Rais ataacha madaraka yake miaka mitano tangu tarehe alipoapishwa kuwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu kwamba Rais Ali Mohamed Shein alikula kiapo cha u-Rais tarehe 3 Novemba, 2010…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tundu Lissu toa hoja.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo naitoa nivumilie tu.

**WABUNGE FULANI:** Aaaaah!

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Kwa hiyo, miaka mitano ya u-Rais wa Ali Mohamed Shein iliisha tarehe 2 Novemba, 2015. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako kama ni jambo linaloruhusiwa Kikanuni kwa mtu ambaye si Rais halali wa Zanzibar, kwa mtu ambaye si Makamu halali wa Rais wa Zanzibar kukaribishwa kwenye siku ya ufunguzi wa Bunge kama Rais au Makamu wa Rais kwa sababu hawa watu si ma-Rais halali, si viongozi halali wa Zanzibar kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar na kwa mujibu wa sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako kama jambo hili linaruhusiwa Kikanuni, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwanza nina taarifa kwamba Rais ameshafika.

La pili, nililoombwa Mwongozo, Mheshimiwa Tundu Lissu ameisoma vizuri Ibara ya 28(2) lakini Ibara ya ndogo ya (1) inasema hivi:-

*"Kufuatana na Katiba hii mtu ataendelea kuwa Rais mpaka:*

*(a) Rais anayefuata ale kiapo cha kuwa Rais". (Makofi/Vigelegele)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kutoa Mwongozo huo kwamba hawa ni viongozi halali mpaka Rais mwingine atakapoapishwa...

**MBUNGE FULANI:** Siyo viongozi halali.

**NAIBU SPIKA:** Nasitisha Bunge mpaka Rais atakapoingia humu ndani.

**MBUNGE FULANI:** Siyo viongozi halali, siyo, siyo.

*(Saa 09.15 Alasiri Bunge lilisitishwa kwa muda)*

*(Saa 9.25 Viongozi wa Kitaifa Walianza kuingia ukumbini)*

*Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Mhe. Mohamed Chande Othman), Jaji Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (Mhe. Omar Othman Makungu) na Spika wa Baraza la Wawakilishi (Mhe. Pandu Ameir Kificho) Waliingia ukumbini*

*(Hapa Wabunge wa Upinzani waliimba kwa sauti Rais ni Maalim Seif)*

*Makamu wa Pili wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (Mhe. Balozi Seif Ali Iddi) Aliingia Ukumbini*

*(Hapa Wabunge wa Upinzani waliimba kwa sauti Rais ni Maalim Seif)*

*Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein) Aliingia Ukumbini*

*(Hapa Wabunge wa Upinzani waliimba kwa sauti Rais ni Maalim Seif)*

*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Mhe. Samia Suluhu Hassan) Aliingia Ukumbini*

*(Hapa Wabunge wa Upinzani waliimba kwa sauti Rais ni Maalim Seif)*

*(Saa 9.45 Alasiri Bunge lilirudia)*

*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Mhe. John P. J. Magufuli) akiongozana na Spika wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Mheshimiwa Job Y. Ndugai) Waliingia Ukumbini*

*(Hapa Wabunge wa CCM walisikika wakiimba kwa sauti CCM na Wabunge wa Upinzani waliimba kwa sauti Rais ni Maalim Seif na wengine kupiga vigelegele)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nawaomba mkae chini.

*(Hapa Wabunge wa Upinzani waliendelea kusimama na kuimba kwa sauti Rais ni Maalim Seif)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nawaomba usikivu.

*(Hapa Wabunge wa Upinzani waliendelea kusimama na kuimba kwa sauti Rais ni Maalim Seif)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mara ya kwanza nawaomba mkae chini.

*(Hapa Wabunge wa Upinzani waliendelea kusimama na kuimba kwa sauti Rais ni Maalim Seif)*

**SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge, kwa mara ya pili nawaomba mkae chini na muwe watulivu.

*(Hapa Wabunge wa Upinzani waliendelea kusimama na kuimba kwa sauti Rais ni Maalim Seif)*

**SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge wote mnaofanya fujo, sasa nawaamuru wote tokeni nje. *(Makofi)*

*(Hapa Wabunge wa Upinzani waliendelea kusimama na kuimba kwa sauti Rais ni Maalim Seif)*

**SPIKA:** Wabunge wote mnaofanya fujo tokeni nje kwa hiari yenu wenyewe. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walisikika wakizomea na wengine wakishangilia)*

**MBUNGE FULANI:** Wazee wazima!

*(Hapa Wabunge wa Upinzani walitii amri ya kutoka nje ya Ukumbi huku wakiimba Rais ni Maalim Seif)*

**MBUNGE FULANI:** Kabakia Zitto. *(Vigelegele)*

**MBUNGE FULANI:** Hapa Kazi tu!

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge wa CCM waliimba kwa sauti CCM, CCM, CCM)*

**SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge, nawaomba mkae na niwahakikishie kwamba 'Hapa Kazi Tu'. *(Makofi/Vigelegele)*

**MBUNGE FULANI:** Waadhibiwe hao, waadhibiwe hao.

*(Hapa baadhi ya Wabunge wa CCM walikwenda kukaa nafasi walizotoka Wabunge wa Upinzani)*

**SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dokta John Pombe Joseph Magufuli amejumuika nasi jioni ya leo ili kutekeleza jukumu la Kikatiba kwa mujibu wa Ibara ya 91(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 ambayo inampa mamlaka ya kulihutubia Bunge Jipya katika Mkutano wake wa Kwanza na kulifungua Rasmi.

Hivyo basi, kwa niaba yenu, naomba nimkaribishe Mheshimiwa Rais wetu mpendwa alihutubie na kulifungua Rasmi Bunge hili la Kumi na Moja. Mheshimiwa Rais, karibu kwa hotuba yako. *(Makofi/Vigelegele)*

**MHE. DKT. JOHN POMBE JOSEPH MAGUFULI - RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA:** Mheshimiwa Job Ndugai, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dokta Ackson Tulia, Naibu Spika; Mheshimiwa Samia Suluhu, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dokta Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar… *(Makofi/Vigelegele)*

Waheshimiwa Marais Wastaafu walioko hapa; Mheshimiwa Balozi Iddi, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar… *(Makofi)*

Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano Wa Tanzania na Waheshimiwa viongozi wote mliohudhuria katika Bunge hili. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, inawezekana ikawa vigumu sana kuwataja wote, lakini nataka nitamke tu kwamba itifaki imezingatiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niko hapa leo kutimiza matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 91(1) inayonitaka kulihutubia Bunge na kulifungua Rasmi Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya njema na kutuwezesha kuwepo hapa siku ya leo. Aidha, nitumie fursa hii kuwakumbuka wenzetu ambao kwa namna na nafasi mbalimbali walishiriki katika mchakato wa uchaguzi huu na kwa bahati mbaya walipoteza maisha yao kabla ya mchakato haujamalizika. Kwa hao wote waliotangulia mbele ya haki, namwomba Mwenyezi Mungu azilaze roho zao na awape pumziko la amani.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kuwapa pole pia ndugu na jamaa ambao ndugu zao walifariki na wengine kupata ulemavu wakati wa mchakato wa uchaguzi huu.

Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwako wewe Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Naibu Spika, Dokta Ackson Tulia kwa kuchaguliwa kwenu kuongoza Bunge la Kumi na Moja, nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli nakupongeza sana na u-Spika wako umeanza kuonekana sasa hivi. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, pia napenda niwapongeze Waheshimiwa Wabunge ambao kwa imani kubwa kwako na kwa Naibu Spika wameweza kuwachagua ili muweze kuliongoza Bunge hili la Kumi na Moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wote, wa vyama vyote, waliochaguliwa kuwa Wabunge wa Bunge hili la Kumi na Moja. Aidha, nitumie nafasi hii kuwapongeza wale wote waliochaguliwa katika nafasi za Udiwani katika kata mbalimbali kote nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natoa pongezi hizi kwa dhati kabisa kwa sababu kuu mbili. Kwanza, ni kwa sababu ushindani katika uchaguzi wa mwaka huu ulikuwa ni mkubwa sana kuanzia ndani ya vyama vyetu na baadaye katika uchaguzi mkuu uliohusisha na kushindanisha wagombea toka vyama tofauti. Pia nawapongeza kwa sababu wananchi wamewapa imani na ridhaa ya kuwawakilisha katika kipindi ambacho matarajio yao kwa Awamu ya Tano ya uongozi wa nchi yetu ni makubwa sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kule kuchaguliwa kwenu kunadhihirisha ni kwa namna gani wananchi wa Tanzania, wa vyama vyote wanavyowaamini na kuwapenda na wana matumaini makubwa kwamba mtawafanyia kazi kubwa. Hongereni sana Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi sote watatupima kwa namna tutakavyokidhi kiu na matarajio yao. Sote tuliahidi kuwatumikia wananchi na kutokana na utumishi wetu kwao, tuweze kutatua matatizo mbalimbali na kuongoza mabadiliko makubwa ya kiutendaji, usimamizi wa matumizi ya mali ya umma na rasilimali za taifa na ugawaji wa rasilimli hizo kwa haki. Mimi pamoja na Mheshimiwa Suluhu, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tuliwaahidi wananchi kuwa tutawatumikia na tutahakikisha kuwa katika utumishi wetu tutawajali wananchi wote bila kujali itikadi za vyama vyao. Zaidi ya wananchi wa kawaida tunaamini na ninyi mliahidi hivyohivyo kwamba mtawatumikia Watanzania wote katika kutatua matatizo yao. Mlichoahidi na daima tukumbuke kuwa kazi zetu na mipango yetu yote tutakayoipanga na kuisimamia italenga katika kuwanufaisha watu wote. Niwahakikishie tu wananchi kuwa mambo tuliyoyaahidi tutayatekeleza kwelikweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sikusudii kurejea mambo yote niliyoyaahidi katika hutuba yangu hii ya leo lakini nataka niwatoe wasiwasi kabisa wananchi wote kwamba tuliyoyaahidi tumeyahidi na ahadi ni deni. Nataka wananchi mniamini kuwa sikutoa ahadi hii ili nipigiwe kura ya kuwa Rais bali niliwaahidi kwa lengo la kuwatumikia na kuwafanyia kazi na hicho ndicho nikachofanya. Ni imani yangu kwamba Waheshimiwa Wabunge pamoja na Waheshimiwa Madiwani pia watafanya hivyohivyo kama ambavyo tumeahidi sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutoa shukrani zangu za dhati kabisa kwa Watanzania wote. Tulijiandikisha kwa wingi sana kwa ajili ya kupiga kura, tulishiriki na kufuatilia kwa karibu sana kampeni za uchaguzi na tukajitokeza kwa wingi siku ya kupiga kura. Kinyume na ilivyotabiriwa na wasiotutakia mema, hakuna siku iliyokuwa ya utulivu mkubwa na amani kama siku ya tarehe 25 Oktoba tulivyokwenda kupiga kura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata baada ya matokeo kuanza kutangazwa, tulionesha utulivu mkubwa na hata pale ambapo matokeo yalipotangazwa na yakawa sivyo kama baadhi yetu waliotarajia bado tuliyapokea kwa hali ya utulivu na uungwana mkubwa. Wale waliotarajia kuwa tutafarakana wameondoka wakiwa wamefadhaika sana huku wakijiuliza hivi hawa Watanzania ni Waafrika wa namna gani? Ndugu zangu, Watanzania kwa mara nyingine tena tumedhihirisha kwetu sisi wenyewe na kwa Afrika na dunia nzima kwamba sisi ni kisiwa cha amani katika bahari iliyochafuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunayo haja ya kujipongeza na kujiwekea nadhiri kuwa tutaendelea kuidumisha hali hii na kuilinda amani ya nchi yetu. Ombi langu kwa vyama vya siasa na wanasiasa wa vyama vyote na viongozi wa dini kutimiza wajibu wetu wa kuilea amani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Zitto ambaye yeye hakulifanyia fujo Bunge lako na yuko hapa. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, hii ndiyo Tanzania nayoitaka. Tanzania ya Watanzania wote, lengo la Watanzania ni kutatua matatizo yao siyo kupiga kelele na kuzomea. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, hili nilitaka nichomekee tu kidogo lakini napenda niungane nanyi pamoja na Watanzania wote kuvipongeza Vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama. Naposema Vyombo vya Ulinzi na Usalama nikimaanisha Jeshi la Wananchi wa Tanzania, Jeshi la Polisi, Magereza, Uhamiaji, Usalama wa Taifa pamoja na Mgambo ambao ni Jeshi letu la akiba hapa Tanzania kwa jinsi walivyoshiriki katika kuhakikisha nchi yetu inaendelea kuwa salama katika kipindi chote cha uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza pia Tume ya Uchaguzi kwa namna walivyosimamia zoezi zima la uchaguzi toka hatua ya awali ya kujiandikisha hadi siku ya kupiga kura na kutangaza matokeo, nawapongeza sana. Wametimiza wajibu wao kwa weledi na umahiri mkubwa katika mazingira magumu na yenye changamoto nyingi, hongereni sana Tume ya Uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, naomba kwa namna ya pekee niwashukuru viongozi wakuu wa nchi yetu waliotangulia kwa kazi kubwa na nzuri waliyoifanyia nchi yetu. Natambua mchango wa Waasisi wa Taifa letu, Mwalimu Julius Nyerere, Mzee Karume, kwa kujenga misingi imara ya umoja, mshikamano na amani ya nchi yetu. Mzee Mwinyi, kwa jina lingine anaitwa 'Mzee Ruksa', kwa kuleta mabadiliko ya kiuchumi na kisiasa na kuijenga misingi yake. Mzee Mkapa au kwa jina lingine 'Mzee wa Ukweli na Uwazi', kwa kupanua na kuimarisha misingi ya uchumi na siasa ya nchi yetu na Mzee Kikwete, ambaye ni 'Mzee wa Maisha Bora', kwa kuendeleza misingi hiyo na kupanua fursa mbalimbali kwa wananchi kujiletea maendeleo yao, wamefanya kazi kubwa. Nawashukuru sana na nawatakia uzee mwema, maisha marefu ili tuzidi kuchuma busara zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeingia kwenye uchaguzi wamoja, tumeshindana katika kampeni tukiwa wamoja na tumemaliza uchaguzi wetu tukiwa wamoja. Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwa ujumla kwamba Serikali ya Awamu ya Tano itaendelea kulinda kwa nguvu na uwezo wote tunu hizi za umoja wa amani. Hatutakuwa na simile kwa mtu au kikundi chochote ambacho kitataka kuvuruga umoja na amani yetu kwa misingi ya udini, rangi, ukabila, vyama au ukanda. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, wakati wa kampeni yako maeneo yaliyojitokeza kwa kulalamikiwa sana na wananchi. Napenda niyataje baadhi ya maeneo yaliyolalamikiwa. Eneo kubwa sana ni rushwa. Suala la rushwa limelalamikiwa sana takribani katika maeneo yote yanayowagusa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine lililolalamikiwa liko ndani ya TAMISEMI. Wanacholalamikia ni upotevu wa mapato, kushindwa kukusanya kodi, ubadhirifu, matumizi mabaya ya fedha na utekelezaji wa baadhi ya miradi chini ya viwango, wizi, uzembe na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine lililolalamikiwa na wananchi wakati tukizunguka tukiomba kura na ninyi Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi, ni ardhi kuhusu migogoro ya wakulima na wafugaji, kuhodhi maeneo bila ya kuendeleza, mipango miji, kujenga maeneo ya wazi na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine lililojitokeza kulalamikiwa ni eneo la bandari. Wananchi wanalalamikia rushwa, wizi, ubadhirifu na urasimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka niyataje haya maeneo yote ili sisi wote tuondoke tukijua kwamba haya ni maeneo ambayo yanalalamikiwa ili tukishatoka hapa tukafanye kazi kwa pamoja kutatua malalamiko haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo limejitokeza kulalamikiwa sana na wananchi ni matatizo ya maji. Wananchi wamelalamikia kiwango cha chini cha upatikanaji wa maji safi na salama lakini huduma za maji kupatikana mbali na makazi na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni *TRA*. Wanalalamika kuhusu ukwepaji kodi, rushwa, ubadhirifu, urasimu na upotevu wa mapato kwa kushindwa kukusanya kodi hasa kodi zinazotakiwa kulipwa na wafanyabiashara wakubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni *TANESCO*. Katika *TANESCO* pamekuwa na suala la kukatikakatika kwa umeme mara kwa mara na kuwepo kwa umeme wa mgao, hilo nalo limelalamikiwa na wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni maliasili na utalii, pamekuwa na ujangili ambao lazima Idara husika inashiriki. Haiwezekani meno ya tembo makubwa kiasi hicho yakashikiwe Ulaya, yamepita hapa bila wahusika wa Idara yenyewe kuhusika kwa aina moja au nyingine. Pia kuna migogoro ya mipaka kati ya vijiji na hifadhi na upotevu wa mapato na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini mengine yaliyolalamikiwa na wananchi wetu ni huduma za afya kwa maana ya hospitali. Huduma kuwa mbali na wahitaji, ukosefu wa dawa, hujuma kwenye vifaa vya vipimo, msongamano wa wagonjwa na tozo zisizostahili, lugha mbaya za watumishi kwa wagonjwa, uhaba wa majengo, uhaba wa vitendea kazi, rasilimali watu na fedha na kushindwa kukusanya mapato yanayowahusu na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, inanibidi haya yote niyataje ili tujue tunaanzia wapi na tunaenda wapi. Nisipoyataja nitakuwa mnafiki na mimi sitaki niwe mnafiki kwa sababu msemakweli ni mpenzi wa Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine linalolalamikiwa ni uhamiaji na ajira. Wanalalamikiwa kwa kutoa ovyo hati za uraia, vibali vya kuishi nchini kwa wageni, kushindwa kusimamia ajira za wageni hususan kwa kazi zinazoweza kufanywa na wazawa na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la elimu nalo limelalamikiwa. Wananchi wanalalamikia suala la elimu kwa kuwa na uhaba wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia, michango mingi isiyo ya lazima, malalamiko ya walimu yasiyoisha, mazingira ya kusomea ikiwa ni pamoja na majengo, madawati, ukosefu wa nyumba za walimu na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo limelalamikiwa ni Polisi. Kuna malalamiko ya wananchi kubambikwa kesi, upendeleo, madai ya askari kutotimizwa, ukosefu wa nyumba za maaskari, ukosefu wa vitendeakazi vya kisasa na kadhalika. Hili pia linaendana na Zimamoto kuchelewa kufika kwenye matukio na wakati mwingine wanapofika kwenye matukio wanatakiwa wafike na maji lakini hata maji hawana na wapo kwenye tukio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni mizani. Kuna malalamiko ya kucheleweshwa kwa magari yanayosafiri katika mizani yetu kwa malengo ya kupata rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mahakama. Natambua jitihada za Mahakama katika kushughulikia suala la mlundikano wa kesi. Hata hivyo, bado kumekuwa na malalamiko mengi juu ya ucheleweshaji wa kesi katika Mahakama zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la madini nalo limelalamikiwa. Wanalalamika wenyeji kutofaidika, vilio vya wachimbaji wadogo wadogo kutengewa maeneo ya uchimbaji na kupatiwa mikopo, kutolipa kodi stahiki, usumbufu wa kulipa fidia na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni kilimo na mifugo. Kuna uhaba wa pembejeo za mifugo na kilimo, tatizo la masoko, kukopwa mazao ya wakulima, ukosefu wa wataalam wa ugani, upungufu wa maghala, mabwawa, malambo, majosho na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la uvuvi napo ni vifaa duni, masoko, uvuvi haramu, uwekezaji mdogo katika sekta ya uvuvi hususan viwanda vya mazao ya uvuvi na kadhalika na hasa katika ukanda bahari. Katika ukanda wa bahari ukianzia Moa kule Tanga hadi Msimbati kule Mtwara kuna zaidi ya kilometa 1,422 lakini katika eneo lote lile la ukanda hakuna viwanda vikubwa vya samaki ambavyo vingeweza kuzalisha uchumi katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni reli. Wanalalamikia kuhusu uchakavu wa miondombinu, kutokuwepo kwa usafiri wa uhakika wa reli, upungufu wa bandari kavu, mizigo mingi kusafirishwa kwa barabara na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni *ATC*. Shirika la Ndege lipo, wafanyakazi wapo zaidi ya mia mbili na wanalipwa mishahara ila ndege ni moja tu wanayohangaika nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni katika makundi maalum, haki za wazee, walemavu, wanawake na watoto zimekuwa zikikiukwa. Pia wafanyakazi wasanii na wanamichezo, mzigo wa kodi kwa wafanyakazi, haki na maslahi yao na kadhalika. Kero hizi ni lazima tuzishughulikie kwa nguvu zetu zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara, Ofisi na Taasisi husika zijipange ipasavyo kutatua kero hizi. Nimezitaja baadhi ya kero hizi ili nanyi Waheshimiwa Wabunge mzitambue na mshikamane na kushirikiana na Serikali na wadau mbalimbali katika kuhakikisha kwamba tunazitafutia majawabu ya haraka.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kero hizo tutashughulikia pia mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, suala ambalo tutalishughulikia ni pamoja na kuimarisha Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilipoapa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania niliapa kuulinda Muungano wa nchi yetu. Hata bila kiapo, mimi ni muumini wa dhati wa Muungano wetu wa kipekee uliounganisha nchi mbili zilizokuwa huru, Nchi ya Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar, tena kwa hiari na kwa wino wa kalamu na siyo mtutu kama ilivyo miungano mingine duniani. Naamini kwa dhati ya moyo wangu kuwa Muungano wetu ndiyo umoja wetu, amani yetu na salama yetu. Ninayo kila sababu ya kuulinda na kuuenzi Muungano wetu adhimu na adimu. Ni azma yangu kuwaona wananchi wa Zanzibar na Bara wakifurahia matunda ya Muungano wetu badala ya kuwa kikwazo kwa ustawi wao na ustawi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na wadau wa siasa hususan vyama vya *CUF* na CCM, tutahakikisha kuwa majaribu ya kisiasa yanayoikabili Zanzibar yanamalizika salama na kwa amani. Tunamuomba Mwenyezi Mungu atujalie busara na hekima tumalize kwa utulivu na amani na Serikali nitakayoiunda itafanya hilo lilo ndani ya uwezo wake kuendelea kuimarisha Muungano wetu. Nina faraja kubwa kuwa Mheshimiwa Samia Suluhu, Makamu wa Rais anao uzoefu mkubwa kutokana na nafasi yake ya awali ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais anayeshughulikia Muungano na pia akiwa Makamu Mwenyekiti wa Bunge la Katiba. Mimi pamoja na Makamu wa Rais, Mama Samia Suluhu na Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, tutahakikisha tunasimamia na kuimarisha Muungano wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo napenda nilizungumzie hapa ni suala la kuimarisha mihimili ya Serikali. Serikali ya Awamu ya Tano itaheshimu na kuendeleza utamaduni mzuri uliojengeka nchini kwa kuheshimu mihimili ya Dola. Tutafanya hivyo kwa kuhakikisha kuwa mihimili yetu ya Bunge na Mahakama inapata fedha za kutosha kuendesha shughuli zake kwa uhuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kupitia Mfuko wa Bunge na Mfuko wa Mahakama, kwa upande wa Bunge tutahakikisha fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo zinapatikana kwa wakati ili Waheshimiwa Wabunge mkashirikiane na wananchi wetu kusukuma maendeleo ya maeneo mnakotoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mahakama tutalipa uzito mkubwa suala la uboreshaji wa Mahakama kwa kusogeza huduma za Mahakama karibu na wananchi na kuongeza kasi ya utoaji haki na kuboresha maslahi ya watumishi wa Mahakama zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la mchakato wa Katiba, Serikali yangu imepokea kiporo cha mchakato wa Katiba ambao haukuweza kukamilika katika awamu iliyopita kutokana na kutokukamilika kwa wakati kwa zoezi la uandikishaji wapiga kura. Napenda kuwahakikishia kuwa tunatambua na kuthamini kazi kubwa ya kizalendo iliyofanywa na wananchi walioshiriki hatua ya awali ya ukusanyaji wa maoni kuhusu Katiba mpya. Pia tunatambua kazi nzuri ya Tume ya Marekebisho ya Katiba na Bunge la Katiba lililotupatia Katiba Inayopendekezwa. Tutatekeleza wajibu wetu kama ulivyoainishwa katika Sheria ya Marekebisho ya Katiba. Napenda mtuamini hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la uchumi na matarajio ya wananchi. Serikali ya Awamu ya Tano inaingia madarakani kukiwa na misingi imara ya kiuchumi iliyojengwa katika awamu inayomaliza muda wake ya Mzee Kikwete. Uchumi wa nchi yetu umekuwa ukiimarika na kukua kwa wastani wa asilimia saba katika kipindi hicho. Fursa mbalimbali za kiuchumi zilizopo nchini mwetu zimezidi kufunguliwa. Hii ni kutokana na jitihada zilizofanywa na Serikali za awamu zilizopita za kujenga miundombinu ya kiuchumi kama vile barabara, uimarishaji wa bandari, uimarishaji wa reli na ukuzaji wa sekta za mawasiliano ya simu na mitandao, ukuzaji na uongezaji wa uwezo wa watu wa kuzalisha na kusambaza umeme. Napenda kuwahakikishia kuwa tutaendeleza na kuimarisha ujenzi wa miundombinu mipya na kuimarisha iliyopo ili kuvutia na kushawishi wawekezaji wa ndani na wa nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu miongoni mwa ahadi tulizowaahidi Watanzania ni kuendeleza ujenzi wa barabara mbalimbali za kuunganisha miji yetu mikuu ya Mikoa na Wilaya, barabara ziendazo kwenye maeneo muhimu ya kimkakati ya kiuchumi na upanuaji wa barabara za miji kama vile Dar es Salaam kwa kujenga *fly over,* barabara za pete na kadhalika.

Uboreshaji wa barabara na njia nyingine za kiuchumi na usafirishaji kuingia na kutoka Dar es Salaam ni muhimu sana kwa sababu bandari ya Dar es Salaam ni lango kuu la biashara kwa nchi yetu na nchi jirani.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada hizo za kuboresha na kuimarisha miundombinu ya kiuchumi, Serikali ya Awamu ya Tano katika kipindi cha miaka mitano ijayo itaongeza nguvu zake katika ujenzi wa reli mpya kwa kiwango cha kimataifa *(standard gauge*). Reli ambazo tumekusudia zianze kujengwa ni ile ya kutoka Dar es Salaam - Tabora - Kigoma hadi Mwanza. Reli ya kutoka Uvinza - Msongati (Burundi) - Isaka - Kigali (Rwanda). Reli ya kutoka Mtwara - Songea - Mbamba bay na matawi ya kwenda Mchuchuma hadi Liganga ambapo ni maeneo ya uzalishaji na pale tunaweza tuka-*boost* uchumi wetu. Pia reli ya kutoka Kaliua – Mpanda hadi Kalema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi yetu pia imejaliwa kuwa na madini na maliasili nyingi. Ugunduzi wa gesi asilia umeongeza matumaini ya watu wengi juu ya uwezo wetu wa kiuchumi katika miaka ijayo. Serikali itahakikisha kwamba madini na maliasili zetu zinatumika kwa manufaa ya Taifa letu kwa kusimamia sheria na taratibu zilizopo.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kuipongeza kwa dhati kabisa Serikali ya Rais Jakaya Mrisho Kikwete na Bunge la Kumi ambapo Mheshimiwa Spika wewe ulikuwa Naibu Spika kwa kupitisha Sheria ya Usimamizi wa Mapato ya Mafuta na Gesi *(The Oil and Gas Revenue Management Act)* ya Mwaka 2015. Serikali yangu itasimamia utekelezaji wa sheria hiyo kwa uaminifu na kwa umakini mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la ujenzi wa viwanda. Serikali ya Awamu ya Tano itaweka mkazo mkubwa katika ujenzi wa viwanda. Natambua kwamba sekta binafsi ndiyo mhimili mkubwa wa kujenga uchumi wa viwanda, hatuna njia nyingine kama kweli tunataka kujenga msingi wa uchumi endelevu katika nchi yetu utakaopaisha uchumi na maisha ya watu wetu. Dira ya maendeleo ya mwaka 2020 inatutaka tuwe nchi ya watu wenye kipato cha kati. Tunaweza tukafika huko na dalili zipo lakini pia tunaweza tukafika huko kitakwimu tu wakati ukweli na uhalisia wa mambo ni tofauti. Utofauti ninaouzungumzia ni pale takwimu zitakapoonesha kwamba sisi ni nchi ya kipato cha kati wakati mapato halisi na hali za maisha za watu wetu hazifanani na takwimu hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tamaa yangu ambayo naamini pia ni tamaa yenu na kwa kweli jitihada za Serikali ya Awamu ya Tano zitakuwa katika kujenga uchumi wa kipato cha kati ambapo sura na maisha ya Watanzania walio wengi yafananefanane na nchi ya kipato cha kati. Njia moja ya kutufikisha huko ni uendelezaji wa viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana tutahakikisha suala la viwanda linasimamiwa vizuri na tunafanikiwa, ndiyo lengo kubwa, kwamba tulisimamie kwa umakini na tufanikiwe. Matarajio yangu ni kwamba Bunge lako Tukufu litatuunga mkono mimi na Serikali nitakayoiunda katika kufikia lengo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema wakati wa kampeni na nataka nirudie hapa kwamba tutaanza na viwanda vilivyopo na kuhakikisha vinafanya kazi. Wale wote ambao walibinafsishiwa viwanda vilivyokuwa vya umma kwa makubaliano kwamba wataviendeleza, niliwataka wafanye hivyo mapema na hapa nataka nisisitize wito wangu huo kwao. Najua huko nyuma ufuatiliaji na usimamizi wa utekelezaji wa mikataba ya aina hiyo umekuwa ukilegalega na watu wamejifanyia mambo wanavyotaka. Wapo walioacha kabisa uzalishaji na kufumua hata mitambo ya uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi niliahidi na nataka niseme hapa kwa wazi kabisa kwamba wale waliobinafsishiwa viwanda hivyo waanze kazi mara moja. Wakishindwa basi tutatwaa viwanda hivyo kwa kuzingatia sheria na taratibu za nchi na kuwapa watu wengine wenye nia ya kuviendeleza viwanda hivyo. Hatuwezi kuwa na watu wanaojiita wawekezaji tunawapa viwanda vyetu halafu wanaviatamia tu kama mayai. Mimi hilo sitalikubali na wala sitalivumilia. Nimeieleza ofisi ya Msajili wa Hazina kuanza kushughulikia suala hili mara moja na naomba Bunge lako Tukufu lituunge mkono katika hili ili tuweze kwenda mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumewadekeza sana, viko viwanda vingine wanafugia mbuzi mle na walipewa kwa misingi kwamba, watakapopewa viwanda vile waweze kuviendeleza, tutengeneze ajira kwa vijana wetu na tujenge uchumi wetu kwenda mbele kinyume chake hawakufanya hivyo. Kwa hiyo, ni lazima tuchukue hatua na hatua tutachukua haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, njia ya pili ya kuendeleza viwanda ni kuhimiza na kushawishi wawekezaji kuwekeza katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Kama nilivyoeleza, miundombinu ya kufanya hivyo tayari ipo na baada ya muda itakuwa bora zaidi. Najua wapo watu wanaotaka kuwekeza Tanzania sasa katika viwanda na wamekuwepo hata miaka ya nyuma kidogo lakini wakati mwingine sisi humuhumu, tukiwemo sisi viongozi kwa kushirikiana na wafanyabiashara matapeli na walaghai tumehujumu mipango ya shauku za wawekezaji wa namna hiyo. Pamoja na shauku na utayari wao wa kuwekeza Tanzania tumewawekea vikwazo na kuwapiga vita na hivyo kuwalazimisha kwenda kuwekeza katika nchi za jirani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi katika Serikali ya Awamu ya Tano tutajitahidi sana kuondoa usumbufu na urasimu wa aina hiyo na kuongeza bidii ya kuwashawishi wawekezaji wa ndani na wa nje kuja kuwekeza viwanda hapa nchini. Hili niseme kwa watendaji wa Serikali ambao kwa njia moja au nyingine watashiriki katika kukwamisha wawekezaji wawe wa ndani au wa nje katika kuwekeza katika nchi hii hatutakuwa na nafasi nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, ni lazima sasa tujue ni viwanda vya aina gani hasa ambavyo tunataka kuviwekeza. Sura ya kwanza ya viwanda tunavyokusudia ni vile ambavyo sehemu kubwa ya malighafi yake itatoka ndani hususani kwenye sekta za kilimo, mifugo, uvuvi na madini na maliasili nyingine. Viwanda vya aina hii tutavipa fursa ya kujenga mfumo wa uzalishaji ndani ya nchi uliofungamana na kushikamana. Viwanda vya aina hii vitahitaji na kutegemea malighafi kutoka kwa wazalishaji wa sekta nilizozitaja hapo mwanzoni na kufanya hivyo wazalishaji hao watakuwa na soko la uhakika humuhumu ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sura ya pili ya viwanda hivi ni kuzalisha bidhaa ambazo zinatumiwa na watu wengi humu nchini yaani *mass consumption* kama vile nguo, viatu, mafuta ya kupikia na kadhalika. Nalizungumza hili kwa sababu nikitoa mfano tu Tanzania tuna zaidi ya ng'ombe karibu milioni ishirini na mbili, au ishirini na tatu na nafikiri ni wa pili baada ya Ethiopia na tunashindana na Sudan lakini hebu angalia bidhaa hata za viatu tu zinazozalishwa hapa, tunaagiza viatu kutoka nje kwenye nchi ambazo hazina ng'ombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tungeweza tukawa na viwanda vya ngozi, tukawa na viwanda vya viatu, viwanda vya mikanda, viwanda vya pochi, viwanda vya kofia na kadhalika. Kwa njia hiyo, tutakuwa tumeongeza thamani ya mazao yetu ya mifugo lakini pia tukawa tumetengeneza au ku-*create employment* kwa watu wetu kwa kuwa na viwanda vya ngozi, viwanda vya viatu na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, viwanda hivi vitakuwa na uhakika wa soko la ndani kabla ya kufikiria soko la nje. Viwanda hivi vitatarajiwa kuzalisha ziada kwa ajili ya masoko ya nje na yote mawili yakitokea yaani kuzalisha kwa ajili ya soko la ndani na nje, itatuongezea akiba yetu ya fedha zetu za kigeni na kutuwezesha kutekeleza na kuendeleza mipango mingine kwa ajili ya ustawi wa uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sura ya tatu ya viwanda navyokusudia ni kuzalisha ajira nyingi. Shabaha yetu ni kuwa ifikapo 2020, idadi ya ajira itokanayo na viwanda ifikie asilimia arobaini ya ajira zote zitakazokuwepo nchini wakati huo. Hii pia ndiyo *reflection* ya Ilani yetu ya Uchaguzi tuliyoinadi sisi wote

Waheshimiwa Wabunge na wananchi kuiamini na ndiyo maana tukachaguliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeamua kulisema hili kwa kirefu sana kwa sababu ili tufanikiwe lazima tuelewane na tusaidiane kulisukuma kwa pamoja jambo hili.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo napenda nilisisitize hapa ni kilimo, mifugo na uvuvi. Sekta nyingine ambazo lazima tutazitilia mkazo mkubwa na kuziendeleza ni kilimo, mifugo na uvuvi. Tutaziangalia sekta hizi kwa mtazamo wa kibiashara na viwanda kwa lengo la kuwa na viwanda vya kisasa vya kuongeza thamani ya mazao yatokanayo na kilimo, mifugo na uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi yetu kwa kiasi kikubwa ni nchi ya kilimo, ufugaji na uvuvi. Hii inatokana na ukweli kwamba sehemu kubwa ya watu wetu wapatao 75% wanaishi vijijini na wanategemea kilimo, ufugaji na uvuvi kwa ajili ya maisha yao. Wakulima, wafugaji na wavuvi wanatumia zana na mbinu duni katika shughuli zao na wanazalisha zaidi ya 95% ya chakula chote kinacholiwa hapa nchini na kutoa mchango wa 25% kwenye pato la Taifa *(GDP)* na 30% ya mapato yetu ya fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, kwa takwimu hizi chache ni wazi kwamba mchango wa sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi katika uchumi wetu na maisha yetu ni mkubwa sana. Nichukue nafasi hii kuwapongeza na kuwashukuru wakulima, wafugaji na wavuvi wote wa Tanzania kwa mchango wao mkubwa katika maisha yetu na uchumi wa nchi yetu. Nataka kuahidi kwao wakulima, wafugaji na wavuvi, sitawaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na umuhimu wa kilimo, mifugo na uvuvi katika uchumi wetu, wakulima, wafugaji na wavuvi wetu wengi bado ni watu maskini, mapato yao yako chini na maisha ni duni. Lengo letu ni kuimarisha sekta hizi ili ziweze kutoa mchango mkubwa zaidi katika uchumi wa nchi lakini pia ziweze kuwanufaisha wakulima, wafugaji na wavuvi katika kuyabadili maisha yao. Tukiweza kuboresha sekta hizi, vijana wengi zaidi watavutiwa kujiunga nazo na hivyo kupunguza tatizo la upatikanaji wa ajira.

Mheshimiwa Spika, nataka niwahakikishie wakulima, wafugaji na wavuvi wetu kwamba ahadi zetu kwao tutahakikisha zinatekelezwa. Serikali ya Awamu ya Tano itazisimamia kwa dhati ahadi hizo ili kuhakikisha kwamba kilimo, ufugaji na uvuvi unakuwa wa kisasa zaidi na wenye tija zaidi. Baadhi ya mambo ambayo tuliyaahidi kuyatekeleza ni pamoja na kuwapatia mafunzo ya kilimo, ufugaji, uvuvi wa kisasa ikiwa ni pamoja na ufugaji wa samaki lakini pia kuwapatia pembejeo wakulima wetu. Tutawapatia zana za kisasa za kilimo, ufugaji na uvuvi, tutawapatia wataalamu wa ugani, tutawawezesha kupata masoko ya uhakika ya mazao yao, tutawapatia mikopo na kwa hili Benki ya

Kilimo itasaidia sana kufikia lengo hili, tutaondoa ushuru wa kodi na kero mbalimbali za mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi zinazosababisha bei ya mazao hayo kuwa chini mfano kahawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakulima wote wa kahawa Kagera wanataka kahawa yao wakaiuze Uganda lakini tulipouliza wana kodi zaidi ya ishirini na sita. Kwa kuzingatia kuwa na kodi hizo zaidi ya ishirini na sita, bei wanayopewa wakulima wa kahawa kule Kagera na maeneo mengine inakuwa ndogo zaidi ukilinganisha na bei wanayopewa katika nchi ya jirani ya Uganda na ndiyo maana wananchi wanachukua *risk* hata ya kwenda kuzama kwenye maji lakini wawe wanasafirisha kahawa. Ndiyo maana nasema kodi hizi za hovyo na ambazo ni kero kwa wakulima wetu katika mazao ya kahawa, mahindi, chai, pamba, korosho, mkonge, ngozi, nyama, maziwa na samaki, tutahakikisha tutaziondoa kama si kuzipunguza kwa kiasi kikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia tutawahakikishia umiliki wa ardhi na kuwaondolea usumbufu wa wao kutokuondolewa kwenye ardhi zao kupisha wawekezaji. Pia tutahakikisha kwamba migogoro ya ardhi baina ya wakulima na wafugaji tunaitatua na kuikomesha kwa kuhakikisha kuwa vyanzo vya misingi vya migogoro hiyo tunaviondoa haraka. Tutahakikisha kwamba tatizo la wavuvi kuvamiwa na majambazi hasa sehemu za Kigoma na uvuvi haramu linashughulikiwa kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika tatizo la umaskini na ajira, nimezungumzia umuhimu wa kuendeleza viwanda, kilimo na uvuvi kwa sababu matatizo makubwa mawili yanayoikabili nchi yetu kwa sasa, kwanza ni tatizo la umaskini na pili ni tatizo la ajira. Ni kweli uchumi wetu umekuwa ukikua kwa kasi ya kuridhisha lakini kasi hiyo haijawiana na kasi ya kuondoa umaskini na uzalishaji wa ajira za kutosha kwa vijana wetu wanaoingia kwenye soko la ajira la kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa takwimu zilizopo, zaidi ya 28.2% ya Watanzania ni maskini na kwamba, kwa namna na kadiri uchumi wetu unavyokua, pengo baina ya matajiri (walionacho) na maskini (wasionacho), linazidi kukua. Tukiendelea hivi tunavyoendelea sasa hatutakuwa tunaitakia mema nchi yetu kwa sababu mgawanyiko mkubwa wa kimapato na tofauti kubwa za kimaisha baina ya matajiri na maskini ukiachwa uendelee na kuzidi kukua utachochea chuki na uhasama baina ya walionacho na wasionacho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni lazima tujizatiti na kutumia akili, maarifa na nguvu zetu zote kukabiliana na kuibadilisha hali hii. Kwanza lazima tushughulike na umaskini wa watu wetu. Njia moja ya kushughulikia hili kama nilivyokwishaeleza, ni uendelezaji wa sekta ya viwanda na uboreshaji wa sekta

za kilimo, mifugo na uvuvi. Tatizo la pili la ajira, kama nilivyokwishakugusia, ukuaji wa uchumi wetu haujaenda sambamba na kasi ya watu wanaoingia kwenye soko la ajira kila mwaka. Tatizo hili la ajira ni kwa vijana wote waliosoma viwango mbalimbali vya elimu na wasio na ujuzi. Hii ina maana kwamba sekta zinazochangia kukua kwa uchumi wa nchi yetu siyo zinazozalisha ajira kwa wingi. Ndiyo maana ya kuweka msisitizo kwenye sekta ya viwanda hasa vile vinavyoajiri watu wengi na sekta ya kilimo, uvuvi na mifugo ambavyo ndivyo mwajiri mkubwa hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuweka msisitizo katika viwanda, kilimo, mifugo na uvuvi, hatuna budi kuwawezesha vijana wetu kuanzisha shughuli mbalimbali za uzalishaji kwa viwango mbalimbali. Ili hili liwezekane na sisi tutalifanya, linahitaji mambo mawili makubwa. Kwanza, kuwaandaa vijana wetu vizuri kielimu na kiujuzi. Hatuna budi kuweka mkazo katika ubora wa elimu na stadi za kazi wanazopata vijana wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nalisema hili kwa sababu hatuwezi kuzungumzia uendelezaji wa viwanda ikiwa hatujaandaa vijana wenye uwezo na ujuzi na stadi za kufanya kazi hizo kwa ubora na ufanisi kwa hali ya juu. Hatuwezi kutaka kuwekeza katika viwanda vya nguo au samani ikiwa hatuna wahandisi wa mitambo wazuri, wabunifu wazuri na wenye viwango vinavyotakiwa kukabiliana na tatizo hilo. Aidha, hatuwezi kuwa na vijana wenye uthubutu wa kuanzisha shughuli za uzalishaji kama hawana elimu na maarifa ya kubuni miradi na kuiendeleza. Kwa hiyo, tutaelekeza nguvu zetu katika kuhakikisha kuwa shule na vyuo vyetu katika ngazi mbalimbali vinafundisha na kutoa vijana wenye viwango vya hali ya juu vya elimu, maarifa, ujuzi na ufundi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili ni suala la wawezeshaji vijana hasa wale watakaotaka kujiajiri. Katika kutekeleza lengo hili, Serikali ya Awamu ya Tano itachukua na kutekeleza hatua mbalimbali ikiwemo kuwawezesha vijana wanaohitimu elimu ya juu na vyuo vya ufundi kupata mitaji ya kuwasaidia kuanzisha makampuni yao kulingana na fani walizozisomea. Pia, tutawawezesha vijana kuanzisha *SACCOs* zao na kupitia *SACCOs* hizo kuwawezesha kupata mikopo. Vilevile, kuwawezesha vijana wajasiriamali kujiunga na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ili waweze kupata mikopo na kunufaika na mafao mengine katika mifuko hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatu ni kuzitambua na kuziheshimu kazi na shughuli mbalimbali zinazofanywa na makundi mbalimbali ya akina mama na vijana. Hapa namaanisha shughuli za akina mama lishe, wachuuzi mbalimbali, machinga, waendesha bodaboda, waendesha maguta na vijana wa kike na wa kiume wanaojitafutia kazi mbalimbali halali za kujipatia mapato kwa ajili ya kuendesha maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, shughuli za makundi haya zinatusaidia sana katika kupunguza makundi ya vijana wetu ambao wangekaa tu na kuzurura hovyo bila shughuli za kufanya. Kwa kuwa, kwa sasa uwezo wetu wa kuwapatia ajira tofauti ni mdogo, ni jukumu letu kuwasaidia na kuwawezesha kufanya shughuli zao kwa utulivu bila bughudha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niliahidi na nataka niahidi na nirudie kusema hapa kwamba Serikali ya Awamu ya Tano ikishirikiana na Halmashauri zetu, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, itaweka mipango na taratibu nzuri na rafiki kwa aina ya shughuli ambazo baadhi nimezigusia. Aidha, ushuru usio wa lazima na wenye usumbufu kwa wafanyabiashara wadogo wadogo utokanao na shughuli nilizozitaja hapo tutauondoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naamini ikiwa tutaweza kuongeza ukusanyaji mapato na kuziba mianya ya wakwepaji wakubwa wa kodi ambao huipotezea Serikali mamilioni na mabilioni ya fedha, tutakuwa hatuna sababu ya kufukuzana na akina mama ntilie na vijana mitaani. Kodi ambazo hatuzikusanyi ni nyingi ambazo zingeweza zikaendesha uchumi wa nchi hii badala ya kukaa na kusumbuana na wanyonge ambao wanajitafutia riziki yao kwa ajili ya kuishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niwatake viongozi wateuliwa walio chini ya mamlaka yangu wakalisimamie hili badala ya kuwanyanyasa wananchi wa hali ya chini wanaojitafutia maisha yao na ikiwezekana waweze kuandaa maeneo maalum kwa ajili ya wao kufanya biashara, hata Ulaya wanafanya hivyo badala ya kila mahali mtu anapokwenda ni kufukuzwa lakini hata wakichukua chakula wanakila wao, kwa hiyo, haya hatuwezi tukayaacha yaendelee kufanyika hivyo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la afya, dhamira ya kujenga uchumi wa kisasa na suala la kupambana na umaskini linakwenda sambamba na kuwa na wananchi wenye afya bora. Kwa kutambua ukweli huu na mahitaji ya huduma bora za wananchi wetu, Serikali ya Awamu ya Tano itahakikisha kwamba wananchi wanapata huduma bora za afya kwa kufanya baadhi ya mambo yafuatayo:-

Kwanza, kuimarisha huduma za afya pale zilipo na kuanzisha pale ambapo hazipo. Lengo ni kuhakikisha kwamba kila kijiji kinakuwa na zahanati, kila kata inakuwa na kituo cha afya na kila wilaya inakuwa na hospitali na kila mkoa unakuwa na hospitali ya rufaa. *(Makofi)*

Pili, tutaimarisha na kuboresha huduma za afya kwa kuongeza utaalam katika nyanja za afya kwa kuwapatia mafunzo watumishi wake ndani na nje ya nchi na kuzipatia vifaa bora na vya kisasa hospitali, vituo vya afya na zahanati

zetu. Lengo la kufanya hivyo ni kuwezesha upatikanaji wa huduma mahsusi hapahapa nchini na hivyo kutolazimika kupeleka watu wetu kutibiwa nje ya nchi. Kwa sababu imekuwa ni kawaida kila mtu akiumwa hata mafua ni kwenda nje wakati kumbe wangeweza kutibiwa hapa vizuri na wakapona na tuka-*save* hela zikatumika kwa mambo mengine ya faida ya nchi yetu. *(Makofi)*

Tatu, tutaongeza bajeti ya dawa na kuboresha mfumo wa upatikanaji ili kuhakikisha dawa zinapatikana katika hospitali, vituo vya afya na zahanati zetu. Aidha, tutahamasisha wananchi wajiunge na bima ya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la elimu, natambua juhudi kubwa zimefanyika katika upanuzi wa elimu ya awali, msingi, sekondari na vyuo vikuu. Serikali ya Awamu ya Tano itajielekeza katika kuongeza ubora wa elimu inayotolewa ikiwa ni pamoja na kuongeza mkazo katika masomo ya sayansi. Aidha, tutahakikisha kwamba vifaa vya kufundishia na kujifunzia vinapatikana ikiwa ni pamoja na maabara, vitabu, madawati na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutahakikisha kuanzia Januari mwakani, elimu kuanzia darasa la kwanza hadi kidato cha nne inatolewa bure. Naposema bure nina maana ya bure. Wahusika wasije wakatumia suala la kusema bure halafu waanze kutengeneza michango ya ajabu ajabu na kuwatoza wanafunzi wale. Ni lazima tuanzie mahali kwamba tunaposema bure maana yake ni bure kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kama tulivyoahidi kwenye kampeni tutahakikisha kwamba wanafunzi wengi zaidi wa elimu ya juu wanapata mikopo kwa wakati. Tutashughulikia maslahi na kero za walimu wa ngazi zote ikiwa ni pamoja na kujenga nyumba za walimu vijijini na kuiunga mkono Benki ya Walimu ili iweze kuwanufaisha zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la maji, wakati wa kampeni nimekutana na malalamiko mengi sana ya ukosefu wa maji. Serikali ya Awamu ya Tano itahakikisha kwamba inaongeza kiwango cha upatikanaji wa maji kufikia asilimia 85 kwa maeneo ya vijijini na asilimia 95 katika maeneo ya mjini ifikapo mwaka 2020. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutakamilisha miradi iliyokwishaanza na kuanzisha miradi mipya mikubwa na midogo ya maji kutoka katika mito, maziwa, vyanzo vingine mbalimbali ambavyo vitakuwa na uhakika wa maji ikiwa ni pamoja na kuvuna maji ya mvua. Tunataka tuwatue akina mama ndoo kichwani. Tunatambua umaskini hauwezi kuondoka nchini kama wananchi hawapati maji safi na salama. *(Makofi/Vigelele)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni la umeme. Suala la upatikanaji wa umeme limeendelea kuwa tatizo katika nchi yetu pamoja na jitihada kubwa zilizofanywa na Serikali zilizopita. Hatuwezi kuzungumzia suala la kujenga viwanda wakati umeme hautoshi. Serikali yangu itahakikisha kwamba umeme wa kutosha unapatikana na wa uhakika. Tutakamilisha miradi ya umeme iliyopo na kujenga mingine mingi mipya ili wananchi wengi zaidi wanufaike na nishati ya umeme na viwanda vingi zaidi vidogo, vikubwa na vya kati viwezi kupata umeme.

Mheshimiwa Spika, pia hujuma zile ndogo ndogo zinazofanywa na watendaji wa sekta ya umeme, kwa mfano, wakati mvua zinaponyesha watu wanalipwa hela pale Mtera wanayafungulia maji usiku halafu *level* yake haifiki kwa wakati kila siku maji hayatoshi, hizi tutazisimamia kikamilifu. Kwa sababu pamekuwa na mtindo huo, watu wanapotaka ku-*supply* majenereta yao au kununua mafuta ya bei ya juu wanalipwa wale wanaohusika pale Mtera kwenye maji, wanayafungulia maji usiku, kwa hiyo, kila siku *level* ya maji inakuwa haifikiwi. Tuta-*deal* nao na mimi nawaambia nita-*deal* nao kwelikweli. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la madawa ya kulevya limekuwa ni janga kubwa kwa Taifa letu na kundi linaloathirika zaidi ni vijana wa kiume na wa kike. Familia nyingi zimeathirika na nguvu kazi ya Taifa imepotea. Tutashughulikia mtandao huo unaojihusisha na madawa ya kulevya bila ajizi. Tutawatafuta wale wakubwa wanaohusika na madawa ya kulevya badala ya kuhangaika na dagaa. Naposema nasema kweli, naomba Bunge mnisaidie na Mungu anilinde na muendelee kuniombea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, masuala mengine tunayoyawekea mkazo katika utawala wa Awamu ya Tano ambayo naamini yatasaidia katika kujenga uchumi wetu ni pamoja na masuala ya utalii, mawasiliano, madini, ardhi, makazi, ujenzi, miundombinu, bandari, barabara, utunzaji wa mazingira, vijana, wanawake, watu wenye ulemavu, wazee, wafanyakazi, wasanii, wanamichezo, wanahabari, wafanyabiashara, wawekezaji, wajasiriamali, sekta binafsi na kadhalika. Ni vigumu kutaja yote tutakayoshughulika nayo katika kujenga uchumi wetu. Utekelezaji wa masuala haya umefafanuliwa vizuri katika Ilani ya CCM ya mwaka 2015. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mapambano dhidi ya rushwa na ufisadi. Jambo moja nililolisemea kwa nguvu kubwa wakati wa kampeni ni mapambano dhidi ya rushwa na ufisadi. Sikufanya hivyo kwa sababu nilitaka tu kuwarubuni wananchi ili wanipe kura zao na kunifanya kuwa Rais wao. Niliongea jambo hili kwa dhati kabisa na nilichokisema na kuwaahidi wananchi ndicho hasa nilichokusudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wanachukia sana rushwa na ufisadi na wamechoshwa sana na vitendo hivyo. Mimi pia nachukia rushwa na ufisadi, sifurahishwi kabisa na vitendo vya rushwa na ufisadi vinavyoendelea hapa nchini. Vitendo vya rushwa na ufisadi vinawanyima haki wananchi na kuitia hasara Serikali kwa mabilioni ya fedha ambazo zingeweza kutumika kwa ajili ya kujenga miradi ya maendeleo kwa ajili ya watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Chama changu cha Mapinduzi kimejengwa katika misingi ya kukataa rushwa na ufisadi. Ndiyo maana moja ya imani kuu za CCM ni ile inayosema rushwa ni adui wa haki sitatoa rushwa wala kupokea rushwa, ingawaje sina uhakika sana kama sasa hivi ndani ya chama chetu hawapokei na kutoa rushwa. Kwa Mtanzania mwaminifu kwa imani yake hatakuwa na kigugumizi katika kuwa mstari wa mbele katika kupambana na rushwa na ufisadi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, mmoja wa Waasisi wa Taifa letu, Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, aliwahi kuifananisha rushwa na ufisadi kama adui mkubwa wa watu. Akiongea Bungeni mwezi Mei, 1960 Mwalimu Nyerere alisema yafuatayo na naomba kunukuu:-

*"Rushwa na ufisadi havina budi kushughulikiwa bila huruma kwa sababu naamini wakati wa amani rushwa na ufisadi ni adui mkubwa kwa ustawi wa watu kuliko vita".* Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya ni maneno makali ya mtu na kiongozi aliyechukia na kuikemea rushwa katika maisha yake yote ya uongozi. Ni maneno yanayotukumbusha tu nini kinaweza kikatokea kama Taifa endapo tutaendeleza rushwa na ufisadi. Chuki za wananchi dhidi ya rushwa na ufisadi ni dhahiri, wamechoka kabisa, wamechoka sana, hawako tayari kuvumilia upuuzi wa Serikali inayoonea haya rushwa na kuleta mafisadi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nimewaahidi wananchi na nataka nirejee ahadi yangu kwao mbele ya Bunge hili Tukufu kwamba nitapambana na rushwa na ufisadi bila kigugumizi na bila haya yoyote. Dawa ya jipu ni kulitumbua na mimi nimejipa kazi ya kuwa mtumbua jipu. Najua kutumbua jipu kuna maumivu lakini bahati mbaya halina dawa nyingine. Hivyo nawaomba Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote, kwanza, mniombee na mniunge mkono wakati ninapotumbua majipu haya.

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge walipiga makofi na vigelegele)*

**MHE. DKT. JOHN POMBE JOSEPH MAGUFULI - RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**: Mheshimiwa Spika, makofi haya yanaashiria kwamba mtaniunga mkono wakati natumbua majipu. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, nafahamu ugumu wa vita niliyoamua kuipigana. Nasema nafahamu ugumu na changamoto zake kwa sababu wanaojihusisha na rushwa siyo watu wadogo wadogo. Vitendo vya rushwa na ufisadi vyenye madhara makubwa kwa nchi na ustawi wa nchi yetu hutendwa na watu wenye dhamana kubwa za uongozi na utumishi ambazo wamezipata kutokana na ridhaa ya watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, ili niweze kufanikiwa lazima nipate ushirikiano mkubwa kutoka kwa Bunge lako Tukufu na vyombo vingine vilivyopo na vyenye majukumu ya kupambana na vitendo hivi vya rushwa. Aidha, tutashinda vita hii endapo wananchi pia watatuunga mkono. Sina mashaka kuwa kwa vile wao wananchi kwa wingi wao wanachukia rushwa na ufisadi watakuwa tayari kutoa ushirikiano wao katika mapambano haya dhidi ya rushwa na ufisadi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo, katika kushugulikia tatizo hili, nimeahidi kuunda Mahakama ya Rushwa na Ufisadi. Ni matumaini yangu, vyombo husika katika jambo hili havitanikwamisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, nataka niahidi mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba kiongozi yeyote wa kuteuliwa ambaye mimi nitakuwa nimeteua kwa mamlaka niliyonayo Kikatiba na ninayo mamlaka ya kumwajibisha pindi tu nikibaini na kujiridhisha kuwa anajihusisha na vitendo vya rushwa pamoja na ufisadi. Nitamtimua mara moja wala sitakuwa na kigugumizi na baada ya mimi kuchukua hatua hizo za kumtimua, taratibu nyingine za kisheria zitafuata. Tunataka twende mbele ili Watanzania wote hasa Watanzania wa maisha ya chini waweze kufaidika na matunda ya nchi yao Tanzania. Tanzania ni tajiri, Tanzania ina kila kitu, tukisimama imara kwa pamoja na tukamtanguliza Mungu mbele tutafanikiwa kwa kuwa na maisha mazuri. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, nachotaka kusema hapa ni kwamba Serikali yangu itafuatilia kwa karibu mienendo ya viongozi na watendaji wake ili kubaini kwa haraka nani anajihusisha na vitendo vya rushwa na ufisadi na tukijiridhisha hatutasubiri, tutachukua hatua. Imani yangu ni kuwa wengine pia katika ngazi mbalimbali mtafanya hivyo hivyo kwa sababu bila kufanya hivyo rushwa na ufisadi vitazoeleka na kuwa wimbo unaoburudisha badala ya kuwa wimbo unaoudhi na kukera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la muundo wa Serikali na utumishi, nilipokuwa nazunguka na kuzungumza na wananchi wakati wa kampeni za uchaguzi, niliahidi nitaunda Serikali ndogo ya wachapa kazi. Aidha, niliahidi pia kuunda Serikali ambayo itawatumikia watu na hasa wananchi wa kawaida. Serikali nitakayoiunda nataka iwe inawahudumia wananchi kwa haraka na siyo kuwasumbuasumbua na kuwazungusha. Natoa rai kwa watumishi wa Serikali hasa ambao ni wazembe na wavivu wajiandae. Tumewavumilia kwa muda mrefu nafikiri wakati wa kuvumiliana sasa umekwisha. Wametuchezea vya kutosha wakati wa kutuchezea sasa umekwisha. Wametuchakachua vya kutosha wakati wa kutuchakachua sasa umekwisha kwa sababu watumishi wa aina hiyo hawatavumiliwa katika Serikali nitakayoiongoza. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, lugha za hiyo ni changamoto, tutashughulikia, tuko kwenye mchakato, tunaendelea, hazitavumiliwa katika Serikali ya Awamu ya Tano. Mimi nataka watu iwe 'Kazi tu'. Hatuwezi kulea watu ambao wanalipwa mishahara lakini hawafanyi kazi wanazotakiwa kufanya au wamegeuza ofisi za umma kuwa ni mahali pa kuchuma bila kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwataka watumishi wa Serikali kufanya kazi hatuna budi kuangalia na kuboresha mishahara na maslahi yao pamoja na mazingira yao ya kufanyia kazi kwa kuwapatia vitendea kazi bora na vya kisasa. Jambo moja tutakalolitekeleza ni kuangalia namna ya kupunguza kodi ya mapato katika mishahara ya wafanyakazi yaani *PAYE*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia tutajitahidi kuwatambua na kuwapa motisha wafanyakazi wachapa kazi ili hii i-*act* kama *motivating agent.* Hata hivyo, kadiri uchumi utakavyokuwa unaendelea tutaangalia pia namna ya kuboresha mishahara yao kwa sababu kila afanyae kazi hana budi kulipwa mshahara mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kuongeza mapato na kupunguza matumizi, kwa zaidi ya miaka mitatu sasa ukusanyaji wa mapato umekuwa chini ya makadirio kwa sababu mbalimbali. Serikali ya Awamu ya Tano itaongeza nguvu katika upanuzi wa wigo wa kodi na kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato. Tutahakikisha kwamba kila mtu anayestahili kulipa kodi analipa kodi stahiki. Hatutasita kumchukulia hatua mtu yeyote atakayekwepa kulipa kodi *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunawaomba wananchi wahakikishe wanapewa risiti kila wanaponunua bidhaa au huduma. Kodi ni kitu muhimu na kimetajwa hata katika Vitabu. Kwa hiyo, ni lazima tulipe kodi na ndiyo maana nasisitiza mtu unaponunua bidhaa ya aina yoyote lazima upewe risiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia tutahakikisha kwamba kila senti inayoongezeka katika mapato ya Serikali inaelekezwa katika kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi. Tutajitahidi kuziba mianya ya upotevu wa fedha za Serikali ambayo inaipunguzia Serikali uwezo wake wa kuwahudumia wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitataja baadhi tu ya maeneo ambayo tutayasimamia kwa lengo la kupunguza matumizi yasiyo ya lazima na kuziba mianya ya upotevu wa fedha za Serikali. Kwanza ni safari zote zisizo za lazima nje ya nchi tutazidhibiti na tumekwishaanza. Badala yake tutatumia Mabalozi wetu kutuwakilisha kwenye mikutano ya aina hiyo na pale inapolazimu kiongozi au mtumishi mwandamizi kusafiri, tutahakikisha kwamba haandamani na msururu wa watu wengi ambao hawana umuhimu wala shughuli za kufanya katika safari hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kusisitiza hili, napenda niwape takwimu za fedha zilizotumika ndani ya Serikali na mashirika ya umma na taasisi nyingine za Serikali kwa safari za nje kati ya mwaka 2013/2014 na 2014/2015 kwa sababu ni lazima niwape takwimu. Jumla ya shilingi bilioni 356.324 zilitumika kwa ajili ya safari za nje kama ifuatavyo:-

(i) Tiketi za ndege (*air ticketing)* zilitumika shilingi billioni 183.16;
(ii) Mafunzo ya nje ya nchi (*training foreign)* zilitumika shilingi bilioni 68.612; na
(iii) Posho za kujikimu (*perdiem foreign)* zilitumika shilingi billioni 104.552.

Mheshimiwa Spika, Wizara na Taasisi zilizoongoza kwa matumizi ya safari za nje ni pamoja na:-

(i) Bunge;
(ii) Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa;
(iii) Wizara ya Fedha;
(iv) Ofisi ya Waziri Mkuu,
(v) Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali *(NAOT);*
(vi) Wizara ya Mambo ya Ndani na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, fedha hizi zingeweza kutumika vizuri kuboresha huduma za wananchi wa maisha ya chini kama afya, maji, elimu na kadhalika. Kwa mfano, fedha hizi nilizozitaja hapa zingetosha kutengeneza barabara ya lami ya kilometa 400. Kwa hiyo, Mheshimiwa Serukamba na barabara yake ya Kigoma ile ambayo kilometa 200 tu zimebaki ingekuwa ni lami, mpaka Uvinza ingekuwa ni lami na tungekuwa tunaelekea Mpanda lakini zimetumika kwa safari za nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini tujiulize zingeweza kutengeneza zahanati ngapi? Zingeweza kutengeneza nyumba za walimu ngapi? Zingeweza kutengeneza madawati mangapi? Zingeweza kununua dawa hospitalini tani ngapi? Hivyo, tunapodhibiti safari za nje, tunawaomba Waheshimiwa Wabunge kwa heshima kubwa sana na Watanzania wote mtuelewe na mtuunge mkono.

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge walipiga makofi)*

**MHE. DKT. JOHN POMBE JOSEPH MAGUFULI - RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA:** Mheshimiwa Spika, pili, tutahakikisha tunadhibiti safari na ziara za mafunzo nje ya nchi zinazogharamiwa na Serikali ambazo zingeweza kupatikana hapa nchini. Unaweza ukawa na utaratibu mzuri tu, badala ya kutuma kikundi cha watu kwenda kufundishwa nje ya nchi mleteni huyo mwalimu anayewafundisha aje awafundishie hapa nchini. Mumlipe mtu mmoja badala ya kulipa kikundi cha watu kwenda kufundishiwa nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini cha ajabu kinachofanyika siku hizi hata bodi *(board meeting)* badala ya kukaa Tanzania kujadili mambo yao wanakwenda Ulaya, ni mambo ya ajabu na aibu. Ndiyo maana ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge napenda mnielewe na ni lazima niliseme, nisipolisema nitakuwa mnafiki na mimi sitaki niwe mnafiki kwani msema kweli ni mpenzi wa Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi wote tuliopo hapa tumewaahidi Watanzania wa maisha ya chini kule tulikotoka, tuwatekelezee yale wanayoyahitaji. Ninyi wote Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi, mmeona shida za wananchi wetu huko vijijini, wana shida kweli kweli. Sisi wote hapa tumeahidi kwamba tutatatua shida zao, hatuwezi tukazitatua shida hizo kwa mtindo huu wa kusafirisafiri na kuwa na matumizi ya hovyo hovyo ndani ya Serikali, Taasisi na sehemu nyingine. Kwa hiyo, napoyasema haya nasema kwa uchungu mkubwa kwamba tuna wajibu wa kufanya haya ili Tanzania yetu ineemeke, ili Tanzania yetu iende mbele, ili wananchi wetu waweze kufaidika, ili wananchi wetu tuwaondolee kero za ajabu ambazo zimekuwa zinawatesa katika maisha yao. Kuna watu wameshasafiri zaidi nje ya nchi kuliko kwenda kumsalimu mama na baba yake kijijini. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, tatu, tutadhibiti warsha, semina, makongamano na matamasha ambayo kwa kweli yanatumia fedha nyingi tu za Serikali lakini hayana tija na wala hayaongezi ufanisi katika utekelezaji na usimamizi wa sera na mipango ya Serikali. Siku hizi kwenye Wizara wakitaka kukutana mahali lazima watafute hoteli wakati Wizarani kuna ukumbi wangeweza hata wakakutania kwenye miti wakazungumza yale wanayotaka kuyazungumza. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nne, tutasimamia kwa ukamilifu Sheria za Manunuzi ya Umma ili kuhakikisha kwamba mianya yote ya upotevu wa fedha za umma tunaiziba. Hii Sheria ya Manunuzi ni mdudu mwingine mbaya, mbaya, mbaya sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unaweza ukakuta nyumba ambayo ingeweza ikajengwa kwa shilingi milioni thelathini kwa Sheria ya Manunuzi itajengwa kwa shilingi milioni mia mbili. Maafisa wetu masurufu wanaokaa kwenye Wizara unaweza ukakuta kalamu ya *Bic* inayonunuliwa kwa shilingi elfu moja imenunuliwa kwa shilingi elfu kumi. Sheria hii imekuwa mbaya kwa matumizi ndani ya Serikali lakini na katika maeneo mbalimbali. Nina uhakika Waheshimiwa Wabunge pakiletwa Muswada wa kubadilisha sheria hii hamtachelewa kuupitisha.

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge walipiga makofi)*

**MHE. DKT. JOHN POMBE JOSEPH MAGUFULI - RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA:** Mheshimiwa Spika, tano, tutasimamia na kudhibiti ukiukaji wa maagizo na maelekezo mbalimbali yaliyokwishatolewa na Serikali siku za nyuma kuhusu ununuzi wa bidhaa kama samani kwa ajili ya matumizi ya Serikali. Samani zote kwa ajili ya matumizi ya Serikali zinatakiwa ziwe zilezile zinazozalishwa hapahapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sita, Serikali ya Awamu ya Tano itasimamia kwa karibu na kudhibiti ununuzi wa magari ya gharama kwa ajili ya viongozi na watumishi waandamizi wa Serikali. Kwa sababu unakuta mtu ni *engineer* unatakiwa uende ukakague barabara badala ya kuwa na *pickup* unataka kununua *V8*, sasa ni lazima tubadilishe huo mwenendo. *(Makofi/Kicheko/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, saba, tutaendelea kuchunguza na kudhibiti matumizi ya Serikali na Taasisi zake zote yasiyo na tija kwa uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, mambo ni mengi lakini kwa ajili hiyo vipaumbele vya Serikali nayotarajia kuiunda vitakuwa ni:-

(i) Kupunguza urasimu ili kuongeza kasi ya utekelezaji wa maamuzi na miradi ya Serikali; *(Makofi)*

(ii) Kubana matumizi kwa kupunguza yale ambayo kutokana na hali yetu ya uchumi kwa sasa yanaweza kuepukika; na

(iii) Kurejesha nidhamu ya Serikali na utumishi wa umma kwa kuongeza uwazi na uwajibikaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutatekeleza vipaumbele hivyo kwa kufanya pamoja na mambo mengine:-

(i) Kupunguza ukubwa wa Baraza la Mawaziri;

(ii) Kuongeza usimamizi katika ukusanyaji wa mapato ya kodi na maduhuli ya Serikali kwa kuziba mianya ya ukwepaji kodi na tutahakikisha kwamba wale wote wanaotakiwa kulipa kodi wanalipa ipasavyo; *(Makofi)*

(iii) Kuongeza nidhamu ya matumizi Serikalini ili kuhakikisha fedha zinazookolewa zinakwenda kwenye miradi ya maendeleo; na

(iv) Kusimamia sheria, kanuni na taratibu za uwajibikaji kwa viongozi na watumishi wa umma ili wawajibike kwa wananchi ambao ndiyo wateja na waajiri wao wakuu wa utumishi na umma.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Tano itaendelea kubainisha maeneo mengine ya matumizi yasiyo ya lazima ambayo yanaigharimu Serikali fedha nyingi na kuyadhibiti. Aidha, nitoe wito kwa Watanzania wote, kila mmoja wetu afanye kazi, awe shambani, ofisini, kiwandani, sokoni, kwenye bustani na kadhalika badala ya tabia ya sasa iliyoanza kujengeka ya Watanzania kutopenda kufanya kazi na hivyo kupoteza muda mwingi vijiweni, muda ambao ungetumika kufanya kazi ndiyo maana kauli mbiu yangu ni 'Hapa Kazi tu'. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu masuala ya mambo ya nje na ushirikiano wa kimataifa, nchi yetu imepata mafanikio makubwa katika nyanja za diplomasia na ushirikiano wa kimataifa katika awamu za uongozi zilizotangulia. Serikali yangu itaendeleza sifa hiyo kwa kujenga juu msingi imara uliowekwa na awamu zilizotangulia na hasa Awamu Nne chini ya Mheshimiwa Dokta Jakaya Mrisho Kikwete. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutaendelea kuwa waumini na tutaendeleza sera ya ujirani mwema na nchi zinazotuzunguka kwa lengo la ustawi wa watu wetu na maslahi mapana ya nchi yetu. Tutaendelea kuwa waaminifu wa utangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na daima tutatekeleza wajibu wetu kwa mujibu wa mkataba wa uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, itifaki zake na maamuzi ya vikao vya nchi wanachama. Tutaendelea kuyatekeleza matakwa na mkataba huu kwa kujenga utengamano wetu hatua kwa hatua.

Mheshimiwa Spika, Tanzania itaendelea kuwa mwanachama mwaminifu wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika *(SADC)* na kuendelea kushirikiana kwa karibu na nchi wanachama ambao tuna mahusiano nao wa

kihistoria na wa kindugu. Pia tutaendelea kuamini katika Umoja wa Afrika na azma ya ndoto wa Waasisi wetu ya kuunganisha Bara la Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutaendelea pia kushiriki kikamilifu katika Jumuiya ya Nchi za Maziwa Makuu *(ICGLR)* na kushirikiana na nchi wanachama wenzetu kutafuta majawabu ya kudumu ya amani, usalama na maendeleo katika eneo la maziwa makuu. Tutaendeleza na kustawisha mahusiano na marafiki zetu wote, magharibi, mashariki ya kati kwa lengo la kushirikiana na maslahi ya nchi yetu kwa watu wetu. Tutapenda kutumia fursa nzuri za mahusiano yetu mazuri kisiasa kukuza mahusiano yetu ya uchumi kwa kutumia diplomasia ya uchumi. Tutafanya hivyo pia kwa ushirikiano wa mataifa kwa kuendeleza mahusiano yetu na Umoja wa Mataifa na taasisi zake, Jumuiya ya Madola, Benki ya Dunia, Shirika la Fedha Duniani, Benki ya Maendeleo ya Afrika (*African Development Bank)* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, aidha, tutazitaka Balozi zetu zioneshe matunda yanayolingana na thamani ya fedha tunazowapelekea hususani katika kuvutia uwekezaji, biashara, utalii, mchango wao katika ukuzaji wa sekta ya viwanda na kadhalika. Tunataka kuona diplomasia na sera yetu ya nje ikijibu changamoto zetu za ndani za ajira, miundombinu, masoko ya mazao ya wakulima, viwanda na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, naomba basi kabla ya kuhitimisha nitoe wito kwa Waheshimiwa Wabunge na Bunge hili ambalo najua linalo nafasi ya kuweka historia ya kuwa kitu kimoja na kuweka maslahi ya taifa mbele. Kama kuna kitu ambacho wananchi wanachukia ni lugha za vijembe, mipasho na ushabiki wa vyama Bungeni. Kwanza, tukumbuke wote bila kujali itikadi za vyama vyetu sisi ni kitu kimoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, tumechaguliwa kuwawakilisha wenzetu. Baada ya miaka mitano kila mmoja atarudi kwenye Jimbo lake kuomba kura na huko atapimwa kwa maendeleo aliyoyapeleka. Ningewaomba tusimame pamoja Tanzania ni yetu sote, tutangulize mbele maslahi ya nchi na kwa mara ya kwanza Watanzania waone Bunge tofauti na siyo Bunge la kuzomea, kutoka nje, kutukanana, mipasho na kadhalika. Ndiyo maana kwa dhati kabisa nimempongeza sana Mheshimiwa Zitto. Mheshimiwa Zitto umekomaa, najua hata kule kwenu Kigoma wamekuchagua wana CCM, ni lazima sasa tujenge dhana ya kutanguliza maslahi ya Watanzania tunaowaongoza badala ya maslahi ya kuzomea, yanaaibisha Bunge hili. Bunge ni chombo muhimu sana katika mihimili ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaitwa Waheshimiwa kwa heshima ya dhamana tuliyopewa na Bunge hili Tukufu, tutunze heshima hiyo ili tuzidi kuheshimiwa.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kusisitiza kuwa kazi iliyopo mbele yetu ni kubwa. Matarajio na matumaini ya Watanzania waliotuchagua na kutupa ridhaa ya kuwaongoza katika kipindi cha miaka ijayo ni makubwa mno, tuna wajibu wa kuyatimiza. Wanachotaka kuona ni nchi yetu kupiga hatua kubwa za maendeleo zitakazojibu matumaini yao na kutatua shida na kero za wananchi wetu. Ninyi na mimi baada ya miaka mitano toka sasa tutapimwa kwa namna tutakavyokuwa tumetekeleza mambo ambayo tumewaahidi Watanzania wenzetu. Mimi nina amini kabisa kwa ushirikiano wetu na kwa kufanya kazi kwa bidii na ubunifu tutaweza kuzitimiza ndoto za Watanzania wenzetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niliona hili nilizungumze kwa sababu na mimi nimewahi kuwa Mbunge katika kipindi cha miaka yangu 20 katika Bunge hili, ninawaomba sana Watanzania wote, ninawaomba sana Wabunge wote, kikubwa ambacho kipo mbele yetu sisi Watanzania ni kutimiza haja za wananchi wetu kwa kuwafanyia kazi, wanahitaji kuona maji yanapatikana, wanahitaji kuona barabara zinajengwa, wanahitaji kuona hospitali zipo, wanahitaji kuona shule zipo, wanahitaji kuona kila kitu ambacho wanakihitaji kwa maisha yao. Sasa tukiutumia muda wetu wa Bunge wakati tuna wajibu wa kuiongoza Serikali itimize wajibu wake, tukafanya mambo kama ambayo yamejitokeza leo ya aibu, hayatatusaidia na kusaidia Watanzania waliotutuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimejitahidi kuzungumza kwa uchache, lakini napenda nikushukuru sana tena, Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa viongozi wote tuliokaribishwa kuingia kwenye ukumbi huu na kushuhudia yaliyojitokeza na mmeona tuna kazi kubwa kwa sababu bado tuna watoto wengi, muendelee kuwavumilia na kuwafundisha na Watanzania wameona. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya napenda sasa kutamka kwamba ninalifungua rasmi Bunge la Kumi na Moja la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Asanteni kwa kunisikiliza! *(Vigelegele/Makofi)*

Mungu libariki Bunge hili, Mungu Ibariki Tanzania, Mungu Ibariki Afrika. Ahsanteni sana. *(Vigelegele/Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, naomba kwa niaba yenu nichukue fursa hii kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano Dkt. John Pombe Magufuli kwa hotuba yake nzuri sana kwetu, inayoweka mwongozo wa kazi kwa miaka mitano ijayo. *(Makofi)*

Ningependa kumuahidi Bunge hili litatekeleza yote yale ambayo ameyaagiza na yote yale ambayo ametuomba na tutakuwa ni mfano wa utekelezaji wa mambo ambayo ameyaelekeza leo. Ninamhakikishia Mheshimiwa Rais kwamba tutakaporudi kwenye kikao kijacho hotuba yake itajadiliwa na Waheshimiwa Wabunge rasmi na kwa kuwa wakati huo tutakuwa tunatengeneza mpango wa utekelezaji wa Serikali wa shughuli zake, tunahakika kabisa mambo mengi tutayaweka katika mpango ili Awamu ya Tano iweze kwenda kama ulivyoelekeza. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maneno hayo ya shukrani naomba sasa nitambulishe wageni tulionao leo hapa Bungeni kama ifuatavyo:-

Katika *gallery* ya Spika tunao Waheshimiwa Marais Wastaafu tukianza na Rais Mstaafu Mheshimiwa Alhaj Ali Hassan Mwinyi, ahsante sana, pia tunaye Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, lakini pia tunaye Rais Mstaafu Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, tunaye Makamu wa Rais Mstaafu Mheshimiwa Dkt. Gharib Mohamed Bilal, tunaye Rais Mstaafu wa Zanzibar Mheshimiwa Dkt. Amani Abeid Karume. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao Mawaziri Wakuu Wastaafu kama ifuatavyo:-

Tunaye Mheshimiwa Joseph Sinde Warioba, tunaye Mheshimiwa John Samwel Malecela, Lakini pia tunaye Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaye pia Mtendaji Mkuu, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Mheshimiwa Ombeni Sefue, tunaye mke wa Mheshimiwa Waziri Mkuu na watoto wake wasimame pale walipo. Tunaye mume wa Naibu Spika, karibu sana shemeji yetu. *(Kicheko/Makofi)*

Tunao wake wa viongozi wastaafu, Mama Fatma Karume, Mama Sitti Mwinyi, Mama Khadija Mwinyi, Mama Anna Mkapa, Mama Shadya Karume, Mama Salma Kikwete, Mama Asha Bilal na Mama Zakhia Bilal, karibuni sana mama zetu. Pia tunaye Mke wa Jaji Mkuu, Mama Saada Chande, tunaye *Dean of Diplomatic Corp*, karibu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, lakini pia tunao Maspika Wastaafu Mheshimiwa Pius Msekwa, karibu sana na Mheshimiwa Mama Anne Semamba Makinda, karibu sana mama. Shughuli uliyoniachia ndiyo hii umeona kidogo leo, tunakushukuru sana. *(Kicheko/Makofi)*

Tunao Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Mheshimiwa Inspekta Jenerali wa Polisi, Mkurugenzi Mkuu wa Usalama wa Taifa, Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa, Kamishna Jenerali wa Magereza, Kamishna Jenerali wa Uhamiaji na Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji. *(Makofi)*

Wageni wengine ni Gavana wa Benki Kuu, Naibu Gavana, Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania na bila kumsahau Makamu Mwenyekiti wa CCM Taifa Mzee wangu Philip Mangula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais, tunao wageni wengine wapo katika kumbi nyingine, ningependa tu kuchukua fursa hii kuwakaribisha wote kwa sababu ya muda, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa nimkaribishe Katibu wa Bunge.

**DKT. THOMAS D. KASHILILAH - KATIBU WA BUNGE:** Hoja ya Kuahirisha Bunge.

## HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE

**SPIKA:** Naomba nimuite Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa Hoja ya Kuahirisha Bunge. *(Makofi)*

## HOTUBA YA MHESHIMIWA MAJALIWA KASSIM MAJALIWA (MB), WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, WAKATI WA KUTOA HOJA YA KUAHIRISHA MKUTANO WA KWANZA WA BUNGE LA KUMI NA MOJA, DODOMA TAREHE 20 NOVEMBA, 2015 KAMA ILIVYOSOMWA BUNGENI

**MHE. KASSIM M. KASSIM - WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya njema iliyotuwezesha kutekeleza majukumu yetu vizuri ya Mkutano wa Kwanza wa Bunge la Kumi na Moja ulioanza tarehe 17 Novemba, 2015. Nimefarijika kuwa kazi zote zilizopangwa katika ratiba yetu tumezikamilisha kwa muda mfupi na kwa umahiri mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii ya awali kukupongeza wewe binafsi kwanza kwa kuchaguliwa na wananchi wa Jimbo la Kongwa kuwa Mbunge wao; na pili, kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi za kishindo kuwa Spika wa Bunge letu la Kumi na Moja la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Nina imani utaliongoza Bunge hili Tukufu kwa kukidhi kiu ya Watanzania ya kutaka Bunge hili litekeleze majukumu yake vizuri, kwa weledi na umakini mkubwa na weledi huu uwawezeshe Watanzania kupata maendeleo endelevu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jana nilikuwa mbele yako, moja kati ya kazi kubwa niliyoifanya ni kushukuru Mungu na kumshukuru sana Kiongozi wetu Mkuu Mheshimiwa Rais. Nataka nitumie pia nafasi hii fupi kumshukuru tena Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa imani kubwa aliyoionesha kwangu kwa kuniteua kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Napenda kumuombea kwa Mungu ambariki, amjalie afya njema na nguvu ya kuwatumikia Watanzania wote, nami ninakuahidi kuwa nitafanya majukumu yote yaliyokusudiwa niyatende katika nafasi uliyonipa na nitatoa ushirikiano mkubwa kwa Watanzania wakiwemo Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, naomba niwashukuru tena Waheshimiwa Wabunge kwa kunithibitisha kuwa Waziri Mkuu wa Kumi na Moja wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kura nyingi hapa Bungeni kwa zaidi ya asilimia 73, hii inaonesha imani kubwa mliyonayo juu yangu na mimi nina imani kubwa juu yenu na kwamba tutashirikiana katika kufanya kazi kwa manufaa ya Watanzania, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile ninawashukuru wananchi wote wa Jimbo la Ruangwa na wengine wapo leo Mjini Dodoma kwa kuwa na imani na mimi kwa kunichagua kuwa mwakilishi wao, napenda kukishukuru pia chama changu Chama cha Mapinduzi kwa kuniteua kuwa Mgombea Ubunge katika Jimbo la Ruangwa na kushiriki katika kampeni zilizoniwezesha kushinda na kuwa Mbunge wa Jimbo hilo la Ruangwa. Bila ya wananchi wa Ruangwa na chama changu nisingekuwa na sifa ya kuwa Waziri Mkuu leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni lazima pia niwashukuru Wazazi wangu kwa malezi na miongozo mbalimbali waliyonipa, iliyoniwezesha kufikia hatua hii ya leo, ninamshukuru pia mwenza wangu Mama Majaliwa na watoto wangu kwa ushirikiano mkubwa, kwa ushauri wake, lakini pia amekuwa mvumilivu kwa muda mrefu wakati wote nikiwa nafanya kazi hii ya utumishi wa wananchi, bila yeye ninaamini nisingekuwa na hamu hata ya kushiriki kwenye shughuli za kisiasa, lakini pia kushiriki shughuli za Watanzania wengine. Ninakushukuru sana Mama Majaliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeendelea kupokea pia salamu nyingi za pongezi kutoka kwa marafiki, ndugu na Watanzania wengine, napenda nitumie nafasi hii kuwashukuru sana Watanzania wote, ndugu wote na marafiki wote ambao wamenipongeza, ninajua changamoto niliyonayo mbele yangu, najua kazi iliyopo mbele yangu ni nzito na yenye majukumu mazito, lakini kutokana na imani kubwa na ushirikiano ambao mmeonesha na imani ambayo mmeionesha pia kwangu na kuahidi kwamba mtanipa ushirikiano mkubwa, ninaamini Mungu atatuongoza wote katika kufanya majukumu haya ya Watanzania. *(Makofi)*

Ninachowaomba wote ni ushirikiano wenu na kwa kuwa mmetanguliza imani kwangu, nami ninaahidi nitafanya kazi kwa bidii, maarifa na uadilifu mkubwa, ili kuwatumikia Watanzania wote bila kujali dini zao, rangi zao na itikadi zao za kisiasa. Ninawaahidi kuwa sitawaangusha na mnajua kwamba awamu hii ya uongozi wa Awamu ya Tano wa nchi yetu ni ya kazi tu, kwa hiyo tutafanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais wetu ameonesha mwelekeo mzuri na mimi nitaitekeleza kaulimbiu hiyo kwa nguvu zote, lakini pia nitaendelea kuihubiri kaulimbiu hii ya hapa kazi na sasa tuseme sasa kazi tu. Ninampongeza sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi punde Mheshimiwa Rais ameeleza kwa kina kuhusu wajibu wetu katika kujenga nchi yetu, ninampongeza Mheshimiwa Rais kwa kutoa hotuba yake nzuri ambayo ndiyo mwongozo wetu katika kuanza kutekeleza majukumu yetu. Kama Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni naomba niseme machache kwa yale aliyoyasema Mheshimiwa Rais na wajibu wetu kama Wabunge.

Mheshimiwa Spika, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lina jukumu moja kubwa la kutunga sheria, sisi kama Wabunge hiyo itakuwa ndiyo kazi yetu ya msingi, lakini ni kazi inayotakiwa kufanywa kwa weledi mkubwa na umakini mkubwa. Ninakumbuka Rais Mstaafu Mzee Benjamin William Mkapa na leo yupo hapa, wakati akifungua Bunge Jipya la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, siku kama ya leo tarehe 20 Novemba, 2000 alitupa methali ya kilatini inayosema na naomba kunukuu; "Mabaya wayafanyayo watu huendelea baada ya wao kutoka duniani, wanaua baada ya wao wenyewe kufa, kwa hisia ya hoja walizozijenga wakiwa hai na kwa sheria walizozitunga." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapoanza kazi hii muhimu, naomba Waheshimiwa Wabunge tukumbuke maneno ya methali hii katika kutekeleza majukumu yetu hasa hili la kutunga sheria. Mimi ninawaombea kila la kheri na fanaka tuwe na busara na hekima katika kufanya kazi zetu na hasa katika kutekeleza jukumu hili muhimu la utungaji wa sheria.

Mheshimiwa Spika, kazi nyingine kubwa ya Bunge kwa maoni yangu ni kuwa karibu na wananchi waliotuchagua. Kuna ukweli kwamba kama Mbunge atafanya kazi yake vizuri ataweza kuwa karibu na wananchi waliomchagua kwa kuwaunganisha na Serikali na kufikisha mawazo yao Serikalini. Aidha, Mbunge mzuri ni yule anayeweza kuwaeleza wananchi kile ambacho Serikali imepanga kukifanya na jinsi ya kutumia rasilimali, fursa mbalimbali tulizonazo, mipango iliyopangwa na watalaam wetu na taratibu zilizopo Serikalini ili kuboresha maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakumbuka pia maneno ya Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa bahati leo wote tunao hapa, alikuwa akifungua pia Bunge la Kumi la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hapa Dodoma tarehe 30 Disemba 2005, alisema na nanukuu: "Ninyi Waheshimiwa Wabunge ndiyo macho na masikio ya wananchi. Mmeaminiwa, na kuheshimiwa, ninaomba kila siku mnapoingia au kutoka katika Bunge hili, mnapozungumza humu ndani au mnaposikiliza mengine wengine wakizungumza, mnapokuwa macho au mnapofumba macho yenu huku mkitafakari kwa kina, kila mara mkumbuke imani na heshima hiyo kubwa mliyopewa na wananchi wetu" Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maneno haya ya hekima ukiyasoma kwa undani kabisa yamebeba hoja na ujumbe mzito kwetu. Ni hoja ambayo tunatakiwa tujikumbushe kila mara katika kipindi chote cha miaka mitano ya uhai wa Bunge letu.

Mheshimiwa Spika, nafahamu kuwa Mheshimiwa Mbunge anakuwa na majukumu mengi lakini kubwa ninalolijua ni utumishi wako kwa waliokupa kura. Wananchi wana mategemeo makubwa sana kwa kila mmoja wetu atajitahidi kuwa nao, ili ashiriki kutatua changamoto mbalimbali za maendeleo na Mheshimiwa Rais kwenye Hotuba yake ameeleza vizuri zaidi. Aidha, ni lazima sisi kama Wabunge kuhakikisha tunashiriki na tunarudi Majimboni na kufanya kazi za wananchi ili kuondoa umasikini na kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kila mmoja wetu hapa anafahamu imani kubwa waliyonayo wananchi kwetu. Ni vyema tukajikita sasa katika kutatua kero zao.

Mheshimiwa Spika, wito wangu kwenu Waheshimiwa Wabunge ni kwamba sasa wote kwa pamoja tushirikiane na Serikali na wananchi wetu waliotuchagua kujenga nchi yetu, ili tuweze kupata mafanikio makubwa na hasa katika kuleta mabadiliko yenye tija. Masuala ya makundi ya kisiasa kati yetu sasa yaishe na tufanye kazi kwa maendeleo na kwa faida ya Taifa letu. Sasa ni Kazi tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wanalo pia jukumu la kuisimamia na kuishauri Serikali ili kuhakikisha kuwa matatizo na kero mbalimbali za wananchi zinatatuliwa. Mheshimiwa Rais, amefafanua kwa kina maeneo yenye kero, aidha kazi ya Mbunge ni kuisimamia Serikali kuhakikisha kuwa inatoa mchango wake kikamilifu katika kuboresha maisha ya wananchi kwa kutumia nguvu kazi, rasilimali tulizonazo, lakini pia ni matarajio ya Serikali kuwa itapata taarifa ya ushauri kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge juu ya maeneo yanayohitajika kupewa msukumo kwenye maeneo yetu ili kuongeza kasi ya maendeleo ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wake Serikali itafanya kazi kupitia taarifa na ushauri tulioupata kutoka kwenu Waheshimiwa Wabunge. Lengo ni kuitoa Tanzania kutoka kwenye dimbwi la uchumi ulionyuma na tegemezi na kuiingiza katika mkondo wa uchumi imara, endelevu, unaokua na wa Taifa linalojitegemea. Jukumu hili ni letu sote Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kila mmoja akifanya kazi kwa kujituma nina imani Taifa letu litasonga mbele na maisha ya watu wetu wote yatabadilika. Mwanazuoni mmoja bwana Ralph Buche aliandika, *"To make our way, we must have firm resolve, persistence, tenacity. We must gear ourselves to work hard all the way. We can never let up."*

Mheshimiwa Spika, anachosema Mwanazuni huyu ni kwamba, tukitaka kusonga mbele kwa mafanikio ni lazima tuweke dhamira ya kweli na tukomae nayo kwa kufanya kazi zaidi, kwa bidii zote, kwa uadilifu mkubwa na Mheshimiwa Rais ameshatutia nguvu mpya ya kwamba "Hapa Kazi Tu." Twende tuweke dhamira na pasiwe na yeyote wa kuturudisha nyuma na yeyote atakayediriki kuturudisha nyuma lazima tuhakikishe tunamrudisha yeye kabla hajaturudisha sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, narudia kuwaombeni kwamba, sasa uchaguzi umekwisha, wote tuseme kwa dhamira moja kuwa yaliyopita si ndwele, tugange yajayo. Twendeni sasa tukashirikiane na wananchi wetu kufanya kazi za maendeleo. Turejeshe ushirikiano na mshikamano miongoni mwetu, tuwasaidie na kuwaongoza wananchi kutatua matatizo yao na wala sio kuwaongoza kwenye mambo yasiyokuwa na tija. Tusibaki tunaanza kutafuta mchawi kumbe mchawi tumemuanzisha sisi wenyewe kwa tabia zetu.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii pia, kuwataka watumishi wote wa Serikali kwa kila mmoja katika eneo lake la utekelezaji wa shughuli za kila siku, malengo ya Serikali ni kupata matokeo makubwa na ya kuleta mabadiliko. Uvivu, uzembe, ubadhirifu wa mali na fedha za umma hautakubalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka niliseme hili na Mheshimiwa Rais amelieleza. Ni vyema kila mtendaji kwa nafasi aliyopewa kuifanyia kazi hatutakuwa na uvumilivu kwa yeyote ambaye hatatekeleza wajibu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Tano imeweka malengo mazuri sana kwa ajili ya utekelezaji. Na tunataka tutekeleze ahadi ambazo Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wakati na baada ya kampeni za uchaguzi, pamoja na Ilani ya Chama cha Mapinduzi na Dira ya Maendeleo tuliahidi mengi na tumeahidi kuwafanyia kazi Watanzania, ili kuleta tija. Hivyo basi tufanye kazi kwa bidii na kuwatumikia Watanzania kwa kasi na umakini wa hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa leo ni Mkutano wa Kwanza na kwa kuwa hiki ni Kikao cha Nne, napenda pia kutumia nafasi hii kuwashukuru wote waliotuwezesha kukamilisha shughuli zilizopangwa kwenye Mkutano huu wa Kwanza wa Bunge la Kumi na Moja kwa ufanisi mkubwa. Ni dhahiri tumeanza vizuri na ninaamini tutaendelea vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi nitumie nafasi hii kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba nitawapa ushirikiano wakati wote wa mijadala ya Bunge hapa ndani. Niwaahidi kwamba nitawatumikia Waheshimiwa Wabunge kwa niaba ya Watanzania wengine, lakini nitawatumikia Watanzania wote kama ambavyo Mheshimiwa Rais amenielekeza, lakini nataka niwahakikishie kuwa nitatembelea kwenye maeneo yenu kuona yale yanayotukabili kwenye maeneo yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, malengo tuliyonayo sasa ni kujenga imani ya Serikali hii ya Awamu ya Tano chini ya Chama cha Mapinduzi kwamba ni Serikali inayoweza kuahidi na kutekeleza. Na Waheshimiwa Wabunge kama ambavyo tumesema awali kwamba ninyi ndiyo washauri wetu, ninyi ndiyo waongozaji, tunatarajia kupata ushirikiano wa dhati kwa kueleza yanayojiri, ili tutende yale ambayo yanapaswa kutendwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nawatakia safari njema za kurudi makwetu, naomba mtufikishie salamu zetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya niseme naweza kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu liahirishwe sasa hadi siku ya Jumanne, tarehe 26 Januari, 2016 saa 3.00 asubuhi, tutakapokutana tena hapa Mjini Dodoma.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**HOTUBA YA MHESHIMIWA MAJALIWA KASSIM MAJALIWA (MB), WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, WAKATI WA KUTOA HOJA YA KUAHIRISHA MKUTANO WA KWANZA WA BUNGE LA KUMI NA MOJA, DODOMA TAREHE 20 NOVEMBA, 2015 KAMA ILIVYOWASILISHWA BUNGENI**

1. **Mheshimiwa Spika,** awali ya yote napenda kumshukuru **Mwenyezi Mungu** kwa kutupa afya njema na kutuwezesha kutekeleza majukumu yetu vizuri ya Mkutano wa Kwanza wa Bunge la Kumi na Moja ulioanza tarehe 17 Novemba, 2015. Nimefarijika kuwa kazi zote zilizopangwa katika ratiba yetu tumezikamilisha kwa muda mfupi na kwa umahiri mkubwa.

2. **Mheshimiwa Spika,** naomba nitumie fursa hii ya awali kukupongeza **wewe binafsi, Kwanza** kwa kuchaguliwa na Wananchi wa Jimbo la Kongwa kuwa Mbunge wao na **Pili,** kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi za kishindo kuwa Spika wa Bunge la Kumi na Moja (11) la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nina imani utaliongoza Bunge hili Tukufu na kukidhi kiu ya Watanzania ya kutaka Bunge hili litekeleze majukumu yake vizuri kwa weledi na umakini mkubwa wa kuwawezesha kupata maendeleo endelevu.

3. **Mheshimiwa Spika,** katika hotuba ya ngu hii fupi napenda kutumia nafasi hii kumshukuru tena Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa imani kubwa aliyoionesha kwangu kwa kuniteua kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Namwomba Mungu akubariki na kukujalia afya njema na nguvu ya kuwatumikia Watanzania. Nami nakuahidi kutoa ushirikiano na kutekeleza yale yote uliyonielekeza. Aidha, naomba niwashukuru tena Waheshimiwa Wabunge kwa kunithibitisha kuwa Waziri Mkuu wa Kumi na Moja wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kura nyingi hapa Bungeni kwa zaidi ya asilimia 73. Hii inaonyesha imani kubwa mliyonayo juu yangu nami ninawaahidi kwamba nina imani kubwa juu yenu.

4. Vilevile, nawashukuru wananchi wote wa Jimbo la **Ruangwa** kwa kuwa na imani nami na kunichagua kuwa mwakilishi wao. Napenda kukishukuru Chama changu Chama Cha Mapinduzi kwa kuniteua kugombea Ubunge katika Jimbo la **Ruangwa** na kushiriki katika Kampeni zilizoniwezesha kushinda na kuwa Mbunge wa Jimbo. Bila Wananchi wa **Ruangwa** na Chama changu nisingekuwa na sifa ya kuwa Waziri Mkuu leo.

5. Ninawashukuru Wazazi wangu kwa malezi na miongozo mbalimbali waliyonipa ambayo imeniwezesha kufikia hatua hii leo. Ninamshukuru Mwenza wangu kwa ushirikiano, ushauri na uvumilivu wake kwa muda wote ambao

nilikuwa nafanya kazi za utumishi wa umma. Bila yeye, naamini nisingekuwa hata na hamu ya kushiriki siasa.

6. **Mheshimiwa Spika,** nimeendelea kupokea salam za pongezi kutoka kwa marafiki, ndugu na Watanzania wengine. **Nawashukuru sana!!** Ninajua kazi iliyo mbele yangu ni nzito na yenye majukumu mazito, lakini kutokana na imani kubwa ushirikiano mliyonionesha na kwa msaada wa Mungu naamini nitaiweza. Ninachowaomba wote ni ushirikiano wenu. Nami ninaahidi nitafanya kazi kwa bidii, maarifa na uadilifu kuwatumikia Watanzania wote na sitowaangusha. Awamu ya Tano ya Uongozi wa Nchi yetu ni ya **Kazi** tu. Mheshimiwa Rais ameshaonesha mwelekeo. Nami nitaitekeleza Kaulimbiu hiyo kwa nguvu zangu zote. **Nampongeza sana Mheshimiwa Rais!**

7. **Mheshimiwa Spika,** hivi punde Mheshimiwa Rais ameeleza kwa kina kuhusu wajibu wetu katika kujenga Nchi yetu. Nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa hotuba yake nzuri ambayo ndiyo mwongozo wetu katika kuanza kutekeleza majukumu yetu. Kama Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni, naomba niseme machache kwa yale aliyoyasema Mheshimiwa Rais na wajibu wetu kama Wabunge.

8. **Mheshimiwa Spika,** Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lina jukumu moja kubwa la kutunga Sheria. Sisi kama Wabunge, hiyo itakuwa ndiyo kazi yetu ya msingi. Lakini ni kazi inayotakiwa kufanywa kwa weledi na umakini mkubwa. Nakumbuka Rais Mstaafu, Mzee Benjamin William Mkapa wakati akifungua Bunge Jipya la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania siku kama ya leo tarehe 20 Novemba, 2000 alitupa Methali ya Kilatini inayosema:

> **"Mabaya wayafanyayo watu huendelea baada ya wao kuondoka Duniani. Wanaua baada ya wao wenyewe kufa kwa hisia ya hoja walizozijenga wakiwa hai, na kwa sheria walizozitunga."** mwisho wa kunukuu.

9. Tunapoanza kazi hii muhimu, naomba Waheshimiwa Wabunge tukumbuke maneno ya methali hii katika kutekeleza majukumu yetu hasa hili la kutunga Sheria. Nami nawaombea kila la kheri na fanaka tuwe na busara na hekima katika kutekeleza jukumu hili muhimu la utungaji sheria.

10. **Mheshimiwa Spika,** kazi nyingine kubwa ya Wabunge kwa maoni yangu ni kuwa karibu na Wananchi waliowachagua. Kuna ukweli kwamba, kama Mbunge anafanya kazi yake vizuri, ataweza kuwa karibu na wananchi waliomchagua kwa kuwaunganisha na Serikali na kufikisha mawazo yao Serikalini. Aidha, Mbunge mzuri ni yule anayeweza kuwaeleza Wananchi kile

ambacho Serikali imepanga kukifanya na jinsi ya kutumia rasilimali, fursa, mipango na taratibu zilizopo za Serikali kuboresha maisha yao. Ninakumbuka maneno ya Rais mstaafu wa Awamu ya Nne Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete alipokuwa akifungua rasmi Bunge la Kumi la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hapa Dodoma tarehe 30 Desemba, 2005, alisema na nanukuu:-

> **"Ninyi Waheshimiwa Wabunge, ndio macho na masikio ya Wananchi. Mmeaminiwa na kuheshimiwa. Naomba kila siku mnapoingia au kutoka katika Bunge hili, mnapozungumza humu ndani au mnaposikiliza wengine wakizungumza, mnapokuwa macho au mnapofumba macho kutafakari kwa kina, kila mara mkumbuke imani na heshima hiyo kubwa mliyopewa na Wananchi."** mwisho wa kunukuu.

11. Maneno haya ya hekima ukiyasoma kwa undani yamebeba hoja na ujumbe mzito sana kwetu. Ni hoja ambayo tunatakiwa tujikumbushe kila mara katika kipindi chote cha miaka mitano cha uhai wa Bunge letu.

12. **Mheshimiwa Spika,** nafahamu kuwa Mheshimiwa Mbunge anakuwa na majukumu mengi, lakini kubwa ninalolijua ni utumishi wako kwa waliokupa kura. Wananchi wana mategemeo makubwa kuwa kila mmoja wetu atajitahidi kuwa nao ili ashiriki kutatua changamoto mbalimbali za maendeleo. Mheshimiwa Rais, kwenye hotuba yake ameliezea vizuri jambo hili.

13. **Mheshimiwa Spika,** Waheshimiwa Wabunge wanalo pia jukumu la kuisimamia na kuishauri Serikali ili kuhakikisha kuwa matatizo na kero mbalimbali za wananchi zinatatuliwa. Aidha, kazi ya Mbunge ni kuisimamia Serikali kuhakikisha kuwa inatoa mchango wake kikamilifu katika kuboresha maisha ya wananchi kwa kutumia nguvu kazi na rasilimali tulizonazo. Ni matarajio ya Serikali kuwa itapata taarifa na ushauri kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge juu ya maeneo yanayohitaji kupewa msukumo ili kuongeza kasi ya maendeleo ya Taifa letu. Kwa upande wake, Serikali itafanyia kazi taarifa na ushauri huo. Lengo ni kuitoa Tanzania kutoka kwenye dimbwi la uchumi ulio nyuma na tegemezi na kuiingiza katika mkondo wa uchumi imara, endelevu, unaokua na wa Taifa linalojitegemea. Jukumu hilo ni letu sote Watanzania. Kila mmoja akifanya kazi kwa kujituma, nina imani Taifa letu litasonga mbele na maisha ya watu wetu yatabadilika. Mwanazuoni mmoja, Bwana **Ralph Bunche** aliandika:

> ***To make our way, we must have firm resolve, persistence and tenacity. We must gear ourselves to work hard all the way. We can never let up!***

14. **Mheshimiwa Spika,** anachosema Mwanazuoni huyu ni kwamba, tukitaka kusonga mbele kwa mafanikio lazima tuweke dhamira ya kweli na tukomae nayo kwa kufanya kazi zaidi na kwa bidii zote na kwa uadilifu wote. Mheshimiwa Rais ameshatupatia nguvu mpya ya kwamba **"Hapa ni Kazi tu"**. Tuweke dhamira na pasiwe na yeyote wa kuturudisha nyuma.

15. **Mheshimiwa Spika,** narudia kuwaombeni kwamba sasa uchaguzi umekwisha, wote tuseme kwa dhamira moja kuwa **"yaliyopita si ndwele tugange yajayo".** Twendeni sasa tukashirikiane na Wananchi kufanya kazi. Turejeshe ushirikiano na mshikamano. Tuwasaidie na kuwaongoza Wananchi kutatua matatizo yao. Tusibaki tunatafuta mchawi kumbe mchawi tumemuanzisha sisi wenyewe kwa tabia zetu.

16. **Mheshimiwa Spika,** napenda kutumia fursa hii kuomba ushirikiano wa Watumishi wote wa Serikali katika kutekeleza Ahadi za Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati na baada ya Kampeni za Uchaguzi, Ilani ya Chama Cha Mapinduzi na Dira ya Maendeleo. Tufanye kazi kwa bidii na kuwatumikia Watanzania kwa kasi na umakini wa hali ya juu. Kila mtendaji afanye kazi kwa sababu hatutakuwa na uvumilivu kwa wazembe.

17. **Mheshimiwa Spika,** napenda kuwashukuru wote waliotuwezesha kukamilisha shughuli zilizopangwa kwenye Mkutano huu wa Kwanza wa Bunge la Kumi na Moja kwa ufanisi mkubwa. Ni dhahiri tumeanza vizuri na ninaamini tutaendelea vizuri!

18. **Mheshimiwa Spika,** baada ya kusema hayo, nawatakia safari njema na naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liahirishwe sasa hadi Jumanne, tarehe **26 Januari, 2016**, saa **Tatu Asubuhi** litakapokutana tena hapa mjini Dodoma.

19. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Nakushukuru sana kwa hotuba yako nzuri. Ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nilipotambulisha wageni nilisahau kuwatambulisha Mabalozi wa nchi za nje waliopo hapa Tanzania, wote kwa umoja wao waliohudhuria nasema karibuni sana.

Waheshimiwa Wabunge, nawaomba sasa tusimame kwa ajili ya Wimbo wa Taifa.

**WIMBO WA TAIFA**

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge waliimba Wimbo wa Taifa)*

**SPIKA:** Ahsanteni, nawaomba mkae kidogo.

Naomba niwatangazie Wabunge kutoka Mkoa wa Tabora kwamba tukimaliza hapa wakutane katika Ukumbi wa Msekwa. Wabunge wa Mkoa wa Tabora mkutane Ukumbi wa Msekwa pale.

Waheshimiwa Wabunge, nimalizie kabisa kwa kukuambia Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Makamu wa Rais na viongozi wote na wananchi wote wa Tanzania; kwanza kukuomba radhi kwa ule utovu wa nidhamu uliotokea kwa kufanywa na baadhi ya wenzetu, Wabunge wenzetu. Tumesikitishwa sana na tabia ile ya kukosa ukomavu. Kipekee kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na uongozi kutoka Zanzibar tunawaombeni radhi sana kwa yaliyotokea.

Nimalizie kwa kusema neno moja tu kwamba niwahakikishie Watanzania kwamba utovu huu wa nidhamu hautaendelea. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mnao uwezo wa kunifanya kuwa Spika mwema, mzuri kabisa, lakini pia mnao uwezo wa kunitengeneza nikawa Spika mbabe kweli kweli. *(Makofi)*

Niwatumie wenzangu hawa walioleta fujo leo *message* kwamba, leo iwe mwisho na ni kwa sababu wazee hawa walikuwepo, lakini siku zijazo hawatakuwepo! Wakifanya tabia kama hii basi, nisiseme sana, iishie hapa hapa! *(Makofi/Kicheko)*

Baada ya maneno haya Waheshimiwa Wabunge, sasa naomba niwahoji kuhusiana na hoja ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu ameitoa hapa mbele yetu kwamba Bunge hili sasa liahirishwe hadi tarehe 26 Januari, 2016.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliafikiwa na Kuamuliwa)*

**SPIKA:** Walioafiki wameshinda. *(Makofi)*

Nawatakia kila la heri, mtakapokwenda huko *christmas* njema, heri ya mwaka mpya, Mwenyezi Mungu atutangulie katika kwenda na katika kurudi kwetu. Ahsante sana. *(Makofi)*

Naahirisha Shughuli za Bunge hadi tarehe hiyo iliyotajwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu.

*(Saa 11.58 Jioni Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Jumanne, Tarehe 26 Januari, 2016, Saa Tatu Asubuhi)*